# ONYO LA MWISHO KWA DUNIA

## MPANGO WA ULIMWENGU MPYA UNAKUJA!

- **Viongozi Wa Ulimwengu Wanautaka**
- **Unao Watetezi Wengi**
- **Ulitabiliwa miaka elfu mbili iliopita**
- **Umekaribia sana**
- **Utauteka Ulimwengu**

- **Ni vipi ya kujiandaa kwa huo mpango**
- **Jinzi ya kuepuka huo mpango**
- **Mwanguko wake wa ghafula na wa mwisho ulitabinwa**
- **Ni wakati wake wa kipekee**
- **Ni mpango mpya halisi**



**"Upende usipende, tayari au la, zote tumehuzishwa ndani na nje, bila kizuizi chochote, katika njia tatu za mashindano ulimwenguni. Wengi wetu si washindani, lakini ni wahusika kwa vile mashindano ni nani atakayeiunda serikali ya kwanza ya muungano, ambayo haijawahi kutokea katika jamii za kimataifa.... Shindano liko nje kwa sababu tayari limeanzishwa, na hakuna njia ya kulirudisha nyuma au kulikomesha". Malachi Martini, *Keys of this Blood,* kurasa 15.❏**

Niwazo Kubwa: mpango mpya wa ulimwengu, wakati mataifa mbali mbali wanapo sukumwa pamoja kwa kusudi la pamoja... ni Marekani pekee ambayo ina msimamo thabiti na uwezo wa kuusukuma mbele. George Bush, asema Katika Gazeti la, *Los Angeles Times*, Feb. 18, 1991.

"Chini ya uongozi shupavu wa Papa Yohana Paulo II, makao Makuu ya Vatikani yaidhinisha mahali pake katika ulimwengu kama sauti ya Kimataifa. Ni haki tu ya kwamba nchi hii ya marekami ndio tu inayoonyesha heshima kwa Vatikani kwa kuielewa kama msuluhishi au mpatanishi na kama taifa katika ulimwengu." Dan Quayle, *Mwito kwa Baraza la Umarekan*i, Septem-ba 22, 1983.

"(Yohana Paulo II) asizitiza ya kwamba watu hawana tumaini la ketegemewa kwa kuiunda serikali inayojitegemea, mpaka tu iwe chini ya msingi wa Ukristo wa Katolika ya Kirumi." M. Martini, *Keys of this Blood*, ukurasa wa 492.

"Umoja wa Mataifa Viongozi wa Kamati ya Ulinzi wa kimataifa walikuwapo hivi leo huko New York katika mkutano wao mkubwa, wakiwa tayari kuiweka Umoja wa nchi za Mataifa kuwa katikati ya mpango huu wa ulimwengu mpya na kuyasukumia mapatano ya umoja kuhusu kulete amani na ulinzi wa silaha....

"Mkutano wa viongozi wa Kamati ya Ulinzi wa nchi 15 ndio wa kwanza tangu mwaka wa 1945 kamati, ilio na uwezo mkubwa wa Umoja wa Mataifa, imekutana katika kilele chake." *Birmigham News*, Jan. 31, 1992.

"Wenzetu tulio wa miaka chini ya sabini twaweza tuk-aona msingi wa serikali ya Ulimwengu mpya ukiwekwa. Wenzetu tulio wa chini ya miaka arobaini hakika hapana shaka kuishi katika utawala wake wa kishenzi, utendaji, na mamlaka sawa. Kweli, watatu hawa wana shindana na muda unapoendelea wengine wengi wengi bali na hawa watatu-wanaongea juu ya mpango wa ulimwengu mpya sio kama kitu ambacho ki karibu sana." M. Martin, *Keys of this Blood*, 15-16.

"Ndoto juu ya Mpango. Kama vile mawazo ya mageuzi mengi, Umoja wa Ulaya sio wazo mpya bali ni la zamani ambalo limefufuliwa. Ndoto la mpango na umoja ulioonekana katika Rumi ya Kaisari ulidumu katika Zama za Kati (au zama za giza) sio tu katika Kanisa la Katoliki la kirumi bali pia katika milki ya Rumi takatifu." *Jarida la Time*, Oktoba 6, 1961.

"Kile ambacho kimekuwa kikisukumwa mbele chini ya Mapatano ya Rumi katika Soko la Pamoja, limefunishwa sana, na hata kunyooshwa sana, na kwa nguvu kuwazuia watawala wa serikali, ambacho ni wazi kabisa ya kwamba kina jaribu kulete msingi wa kiuchumi wa Milki ya Rumi Takatifu katika ulaya." *Christian Science Monitor*, 1962.❏

## *MAREKANI - UPAPA - UMOJA WA MATAIFA*

## JE RUMI ITATAWALA ULIMWEGU TENA?

*Sio juhudi la jarida hili kushambulia watu binafsi bali ni kutoa historia na kibibilia unabii uliotabiriwa katika mpangilio wa dini ya Kikatoliki siku za usoni.*

# MAPATANO YA KIFO

MTUME PAULO, katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike, alitangulia kutabiri juu ya uasi mkuu ambao matokeo yake yangeleta kusimamishwa kwa uwezo wa kipapa. Alitangaza kwamba siku ya Kristo haitakuja, "usipokuja kwanza ule ukengeufu, akafunuliwa yule mtu wa kuasi mwana wa uharibifu; yule mpingamizi ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho mungu, au kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." Na zaidi ya hapo, mtume paulo alionya wandugu wake wa imani kwamba "maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi." 2 Wathesalonike 2:3-4,7. Hata mwanzo wa nyakati hizo, aliyaona yakinyemelea kuingia kanisani, makosa ambayo yangeandaa njia kwa kukua kwa upapa.

Kidogo kidogo, kwanza kwa siri na kimya, na wazi zaidi ilipokuwa ikiongezeka kwa nguvu na kuyatega mawazo ya watu, "siri ya uasi" iliendeleza mbele udanganyifu wake na kazi yake ya makufuru. Karibu kutoonekana kabisa mila za kishenzi zikapata mahali kuingia katika kanisa la Ukristo. Ile roho ya mapatano na kufanana ilizuiliwa kwa muda na mateso makali ambalo kanisa lilifumilia chini ya kishenzi. Lakini mateso ilipokoma, na Ukristo kuingia majumba ya wafalme, kanisa likaweka kando unyenyekefu wa kristo na mitume wake kwa kujitakia makuu na kiburi ya makuhani na viongozi wa kishenzi; na katika sehemu ya sheria ya Mungu, badala yake likabandilisha elimu na mafundisho ya watu. Kuongoka nusu kwa Costantino, katika mwanzo wa karne ya nne, kulileta shangilio mkubwa; na ulimwengu, ukiwa umefunikwa mfano wa nguo ya haki, ukaingia kanisani. Sasa kazi ya uharibifu ikaendelea mbele kwa kasi. Ushenzi, ulipoonekana kushindwa, badala yake ukashinda. Roho wake akatawala kanisa. Mafundisho yake, sherehe zake, na mambo ya uchawi vikashirikishwa katika imani na ibada za wanaokiri kuwa Wakristo.

### *Mtu wa Kuasi*

MAPATANO hayo kati ya kishenzi na Ukristo yalitokea kustawi kwa yule "mtu wa kuasi" aliyetabiriwa katika unabii kuwa mpingamizi ajiinuaye nafsi yake juu ya Mungu. Utaratibu huu wa dini ya uongo ni kazi bora ya nguvu za Shetani-ni nguzo ya juhudi yake yeye mwenye kukaa katika kiti kuitawala dunia kulingana na mapenzi yake. Shetani alijitahidi awali kufanya mapatano na Kristo. Alimjia Mwana wa Mungu katika jangwa ya majaribu, akimwonyesha Yeye falme zote za ulimwengu na utukufu wake wote, akamuahidi kutoa vyote mikononi Mwake ikiwa Angekiri utawala wa huyu mfalme wa giza. Kristo alimkemea mshawishi huyo mwenye kiburi na kumtukuza. Lakini Shetani huleta majaribu hayo kwa mwanadamu. Kwa kupata faida za ulimwengu na heshima, Kanisa likaongozwa kutafuta upendeleo na dunia; na baada ya kumkana Kristo, akashawishiwa kutoa utiifu kwa mwakilishi wa Shetani askofu wa Rumi.

### *Msingi wa Upotovu*

NI MOJA yapo ya mafundisho tangulizi ya Kirumi ya kwamba papa ndiye kichwa halisi cha kanisa la Kristo ulimwenguni, ambaye amezingirwa na uwezo wa utawala juu ya maaskofu na wachungaji katika pembe zote za ulimwengu. Zaidi ya hayo, papa amepewa jina la Mungu. Amekuwa akiitwa kwa umbo la "Mungu Bwana Papa," na amekuwa akinenwa kuwa asiyeanguka. Yeye hutaka watu wote wamsujudie. Dai lile lile Shetani alisisitiza katika jangwa la majaribu anaendelea kusisitiza kupitia Kanisa la Rumi, na idadi kubwa ya watu wako tayari katika heshima zake.



Church of St. Peter, Rome

Lakini wamchao Mungu na kumheshimu hukumbana na madai haya ya kujiinua-juu ya Mbinguni kama vile Kristo alivyo kumbana na ushawishi wa yule mjanja: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake." Luka 4:8. Mungu hajawahi kudokeza katika Neno Lake ya kwamba Yeye amemteuwa mtu ye yote kuwa kichwa cha kanisa. Fundisho la utawala wa kipapa hupinga kabisa mafundisho ya Maandiko. Papa hawezi kuwa na nguvu juu ya kanisa la Kristo ila tu kwa unyang'anyi.

> **"Hapa duniani tunashikilia pahali pa *Mungu Aliye Juu.*"**
> **Papa leo XIII, Katika barua kitabu cha maarifu juni 20 1894.**

Warumi wameshikilia katika kuleta uzushi juu ya Waprotestanti na kujitenga katika kanisa la kweli. Lakini lawama hizi zina walenga hao wenyewe. Hao ndio walioi-shusha chini bendera ya Kristo na wakajitenga na "imani iliokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Jude 3.

### *Vumbuzi la Uongo*

SHETANI alijua sawa kabisa ya kwamba Maandiko Matakatifu yangewezesha watu kutambua udanganyifu wake na kupinga nguvu zake. Ni kupitia kwa Neno hilo Mwokozi wa ulimwengu alizipinga shambulizi zake. Katika kila shauri la yule adui, Kristo alitoa kinga la ukweli wa umilele, akisema, "imeandikwa." katika kila shawishi la yule adui, Aliupinga akitumia hekima na nguvu ya Neno. Ili Shetani audumisha mvuto wake juu ya watu, na kusimamisha uwezo wa unyanganyi wa kipapa, ni mpaka angefanya wasiyajue Maandiko. Bibilia ingemwinua Mungu na kuwaweka wanadumu katika mahali pao halisi; kwa hivyo, kweli za Bibilia zingefichwa na kukanyagiwa chini. Na elimu hii ilibuniwa na Kanisa la Kirumi. Kwa mamia ya miaka usambazaji wa Bibilia ulikataliwa. Watu walikatazwa kusoma au kuwa nayo manyumbani mwao, na makuhani wasio na msingi na maaskofu wakatafsiri mafundisho yake ili kutosheleza ubinafsi wao. Kwa hivyo papa akawa Mungu duniani, ambaye amevikwa mamlaka juu ya kanisa na serikali.❏

# KUSUJUDU KISHENZI

FUMBUZI la uogo lilipo-ondolewa, Shetani akafanya kulingana na mapenzi yake. Unabii ulikuwa umetangaza kwamba Upapa "ungefikiria kubadili maji ra na

sheria." Danieli 7:25. Jitihada hii haikujaribiwa pole pole. Ili kujipatia waumini kutoko kwa mataifa badiliko la ibada ya sanamu, na hasa kuinua Ukristo wao wa jina tu, ibada ya sanamu na makumbusho ya wafu iliingizwa pole pole katika ibada ya Wakristo. Amri ya kamati kuu mwishowe ikajenga utaratibu huu wa uabuduaji wa sanamu. Ili kukamilisha kazi hii ya kukufuru, Rumi ikawazia kuiondoa kutoka kwa sheria za mungu amri ya pili, inayokataza uabuduaji wa sanamu, na kugawanya amri ya kumi, ili waendelee kuwa na hesabu kamili.

### Sheria za MUNGU

I

Usiwe na Miungu mingine ila mimi.

II

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukioa, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

III

Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

IV

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanye mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

V

Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.

VI

Usiue

VII

Usizini

VII

Usiibe

IX

Usimshuhdie jirani yako uongo

X

Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.

Kutoka 20:3-17

### Sheria Ta mungu iuvtobad na mwanadamu

I

Mimi ndimi Bwana mungu wako. usiwe na miungu mingine ila mimi.

(Amri ya pili Imeondolewa)

II (III)

Usilitaje bure jina la Bwana mungu wako (hakika ni ta tatu)

III (IV)

Uikumbuke kuitunza kwa utakatifu siku hii ta sabato (kwa hakika ni ya nne, na sheria hii ya sabato imegeuzwa kabisa)

IV (V)

Waheshimu baba na mama (hakika ni ya tano)

V (VI)

Usiue (kwa hakika ni ya sita).

VI (VII)

Usizini (kwa hakika ni ya saba).

VII (VIII)

Usiibe (hakika ni ya nane).

VIII (IX)

Usimshuhudie jirani yako uongo (kwa hakini ni ya tisa, sehemu ya kwanza)

IX (Amri ya X sehemu ya kwanza)

Usimtamani mke wa jirani yako (hakika ni ya kumi, sehemu yake ya kwanza)

X (Amri ya X sehemu ya pili)

Usitamani mali ya jirani yako (hakika ni ya kumi Sehemu yake ya pili)

**Katekisimu ya wakatoliki wote.**

### Mapatano Yaendelea

ROHO WA kukubali mambo ya kidunia iliendelea kufungua njia zaidi ya kupuuza uwezo wa Mbinguni. Shetani, akifanya kazi kupitia kwa viongozi waasi wa kanisa, wakaiharibu pia sheria ya nne, na kuijaribu kuweka kando Sabato ya zamani, siku ambayo Mungu aliibariki na kutakasa (Mwanzo 2:2-3), na badala yake kuinua siku ya sherehe ilyokuwa inatunzwa na mataifa kama "siku ya heshima ya juu." Kwa mara ya kwanza badiliko hili halikujaribiwa dhahiri. Katika karne za kwanza Sabato ya kweli ilitunzwa na Wakristo wote. Walikuwa na wivu kwa heshima ya Mungu, na, wakiwa na imani ya kwamba sheria yake, ni imara, kwa juhudi wakatunza usafi wa maagizo yake. Lakini kwa ujanja mwingi Shetani akafanya kazi kupitia kwa waakilishi wake ili kutimiza lengo lake. Ili mawazo ya watu yapate kuvutwa kwa Jumapili, ikafanywa kuwa ni siku ya sherehe kwa kuheshimu ufufuo wa Kristo. Mikutano ya kidini ilifanywa katika siku hiyo; na huku siku hiyo ilitunzwa kama siku ya burudiko, huku Sabato ikiendelea kutunzwa. Kwa kuiandaa njia ya kazi yake alioipanga kuikamilisha, Shetani kabla ya kurudi kwa Kristo, alikuwa amewaongoza Wayahudi, kuilemesha chini Sabato na maagizo magumu, kwa kuifanya utunzaji wake kuwa mzigo. Sasa, kwa kuiichukulia nafasi ya nuru ile ya uongo ile aliowafanya wengi kuiamini, akatoa dhihaka juu yake akasema eti ni sheria ya Wayahudi. Kwa kawaida Wakristo wanapoendelea kutunza Jumapili kama sherehe ya furaha, akawaongoza, ili apate kuwaonyesha uadui dhidi ya Wayahudi, kwa kuifanya Sabato kuwa siku ya kufunga, huzuni na siku ya utusitusi. ❑

# BADILIKO THUBUTI

MWANZO wa karne ya nne mfalme Costantino aliipitisha sheria ya kuifanya Jumapili kuwa ya sherehe ya wote katika enzi ya Kirumi. Siku ya jua iliheshimiwa na wafuasi wa kipagani na Wakristo pia; zilikuwa hila za mfalme kuunganisha Wakristo. Alisukumwa kufanya hili na maaskofu wa kanisa, waliokuwa, na tamaa na kiu ya utawala, wakifikiria ya kwamba siku hiyo ikiabudiwa na wote Wakristo na watu wa mataifa, ingeinua ukubaliaji wa Ukristo nusu ya upagani na kwa hivyo kuendeleza uwezo na utukufu wa kanisa. Lakini huku wengi wa Wakristo wacha-Mungu walisukumwa pole pole kuitakasa Jumapili kama siku takatifu, na pia waliishikilia Sabato ya kweli kuwa takatifu kwa Bwana, na wakaitunza kulingana na utiifu wa amri ya nne. Mdanganyifu mkuu hakuwa amemaliza kazi yake. Alinuia kukusanya ulimwengu wa Wakristo chini yake na kudhihirisha nguvu zake kupitia kwa huyo mdanganyifu anayedai kuwa mwakilishi wa Mungu duniani, askofu huyo mwenye kiburi anaye dai kuwa mwakilishi wa Kristo. Kupitia kwa wapagani walioongoka nusu, maskofu wenye tamaa, na watu wa kanisa waupendao ulimwengu Shetani akalikamilisha kusudi lake. Mikutano mikubwa ilifanywa mara kwa mara, ambayo wakuu wa kanisa walikusanyika kutoka ulimwengu kote. Na katika kila kikao Sabato iliyowekwa na Mungu ilishushwa chini kidogo, huku Jumapili ikiinuliwa juu. Kwa hivyo siku ya sherehe ya kipagani ikaja kutukuzwa na kuheshiwa kama siku takatifu, huku Sabato ya Bibilia ikakanyagiwa chini kuwa mabaki ya Wayahudi, na walioendelea kuiabudu wakatangazwa kuwa wamelaaniwa.

### Kuondolewa kwa Muhuri wa Muumbaji

MUASI MKUU alishinda kwa kujiinua mwenyewe "kwa cho chote kiitwacho Mungu, au kuabudiwa." 2 Thesalonike 2:4.

**"Jumapili ni amri ya kikatoliki, na uabuduaji wake waweza kuhifadhiwa tu chini ya misingi ya kikatoliki.... toka mwanzo hadi mwisho wa maandiko hapana kurasa hata moja inayodhihirisha badiliko hili la ibada ya kila juma toka siku ya mwisho ya kwanza" *Chapa ya Katolika* Sydney, Australia Agosti 1900.**

**Sabato ilitunzwa na wakristo wote katika karne za kwanza.**

**"Ya kwamba kanisa la kirumi limemwaga damu isiyo na hatia kuliko kanisa lolote ambalo limewahi kuweko katikati ya mwadamu."** W.E.H. Lecky. *Historia ya kuinuka na mvuto wa elimu ya binadamu kule uroba* sehemu ya 2 kuraza ya 62, 1910.

**Ni kisio hesabu ya vifo 40,000 vya wakristo ambao huwawa kila mwaka wakati upapa huwepo,** *Historia ya Kirumi,* kurasa za 541-542.

Amejaribu kubadili amri ya pekee katika sheria za Mungu ambayo dhahiri inawaelekeza watu kwa Mungu wa kweli aishie. Katika sheria ya nne, Mungu amedhihirishwa kama Muumbaji wa mbingu na nchi,na hivyo basi kubainishwa kutoka miungu mingine ya uongo. Ilikuwa ni ya kumbukumbu ya kazi ya Umbaji ili siku ya pumziko kwa mwana-damu. Ilikuwa ni kusudi la mhifadhi Mungu aishie daima katika mawazo ya watu kama muumbaji wa viumbe vyote na anayefaa heshima na Ibada. Shetani hupigana vita kuwageuza watu kutoka kwa utiifu wao kwa Mungu, na pia wanapoonyesha utiifu kwa sheria Zake; hivyo basi anaelekeza juhudi zake hasa juu ya sheria inaonyesha Mungu kama Muumbaji.

Madhehebu ya Waprotestanti yanasisitiza kuwa kufufuka kwa Kristo katika siku ya Jumapili ndio ilifanya siku hiyo kuwa Sabato ya Wakristo. Lakini hapo hakuna ushahidi wa Maandiko. Kristo hakutoa heshima kwa siku hiyo wala wanafunzi Wake pia.

### Toka Rumi ya Kishenzi Hadi Rumi ya Kipapa

KATIKA karne ya kumi na sita utawala wa Kipapa ulikuwa umesimama imara. Na askofu wa Rumi akatangazwa kuwa kichwa cha kanisa kwa jumla. Dini ya Kishenzi ilitoa nafasi kwa Upapa. Yule joka alikuwa amempa myama "nguvu zake, na kiti chake cha enzi, na uwezo mwingi." Ufunuo 13:2. Na hapo ndipo ikaanza ile miaka 1260 ya mateso ya kipapa iliotabiriwa katika unabii wa Danieli na Ufunuo. Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7.

Wakristo walilazimishwa kuacha unyofu wao na kukubali sherehe za kipapa na ibada, au sivyo kuyaharibu maisha yao katika gereza ama kuuwawa kwa kutundikwa, au kutundikwa kwa miti, au kwa kuuwawa na shoka. Ndipo sasa ikatimia maneno ya Yesu: "Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu, na ndugu zenu, na jamaa yenu, na rafiki zenu; na watawafisha baadhi yenu. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu." Luke 21:16-17. Na mateso yakaenea kwa watakatifu kwa hasira nyingi kuliko hapo awali, na ulimwengu ukawa kiwanja kikubwa cha vita. Kwa mamia ya miaka kanisa la Kristo lilipata kimbilio katika mafichoni na mahali penye giza. Basi asema nabii: "Yule mwanamke akakimbia nyikani, ambapo ana mahali iliotayarishwa na Mungu, ili wamlishe huku muda wa siku elfu na mia mbili na sitini." Ufunuo 12:6.❏

# ZAMA ZA GIZA ZAANZA

**"Kwa kichwa cha mfalme wa mji mkuu wa vatikani na kile cha kanisa katoliki la kirumi, karoi wojtyla (yaani papa yohana) ajadilia namna ya uwezo ambao ungegawanywa kati ya wanabiashara katika mambo ya ulimwengu." Kweli kanisa lake lilikuwa na waongovu nusu zaidi ya milioni 907 ambao ni karibu asilimia kumi na nane ya watu katika ulimwengu wa sasa. Alikuwa na makuhani 483, 488 na karibu maaskofu watukufu 3,000 watumikiao vituo vya makuhani 211, 156 ambayo vinaunda majimbo 1,920 duniani na majimbo makubwa 513. Shirika lake la Muungano limejumulisha shule za misingi, vyuo vikuu, majengo ya uchuuguzi, vituo vya sayansi na matibabu kwa watu wote, mahospitali, nyumba za watawa makanisa, makanisa makuu ya majimbo ya askofu, makanisa madogo, vituo vya kidini, majumba ya ubalozi, majumba ya kuhifadhi hati na tarehe, maktaba, sanaa, magazeti. Bohari, majumba ya uchapishaji, vituo vya redio na televisheni. Kwa hakika tena, Anashikilia Benki yake mwenyewe ya vatikani, pamoja na kundi lake la washauri wa kimataifa wanaohudumia katika farada ya barua katika mashamba na akiba ndani ya kila sehemu ya ulimwengu wa biashara na uchumi. *Keys of this Blood*, kurasa 111, M. Martino.**

KUTAWAZWA kwa Kanisa la Kirumi kwa mamlaka ndiyo ulikuwa mwanzo wa Zama za Giza. Jinzi nguvu zake zilivyoongezeka, giza ikaongezeka. Imani ikahamishwa kutoka kwa Kristo, ambaye ni msingi wa kweli, mpaka kwa papa wa Kirumi. Badala ya kumtumainia mwana wa mungu kwa msamaha wa dhambi na wokovu wa milele, watu wakamuangalia papa, na makuhani na maaskofu ambao papa aliwapa uwezo huo. Walifunzwa ya kwamba papa ndiye mpatanishi wao hapa dunia na hakuna mtu angemkaribia Mungu ila kupitia kwake; na, zaidi hasa, kwa kusimama pahali pa Mungu kwa ajili yao angepaswa kuabudiwa kikamilifu. Kujitenga kutoka kwa maagizo yake ilikuwa sababu ya kutosha kwa mateso makali ambayo yangewaangukia miili na roho ya waasi. Kwa hivyo mawazo ya watu yakageuzwa kutoka kwa Mungu hadi anayeanguka, wakosaji, na wakatili, hasa na, zaidi, kwa mkuu wa giza mwenyewe, ambaye huonyesha nguvu zake. Dhambi ikafunikwa katika nguo ya utakatifu. Wakati Maandiko yanapokanyagiwa, na mwana-damu kujifanya kuwa kama Mungu, twahitaji kutazamia tu ulaghai, udanganyifu, na uasi wa ufisadi. Kwa kuinuliwa kwa sheria za mwanadamu na desturi ilidhiihirisha uharibifu ambao hutokea kwa kuweka kando sheria ya Mungu.

### Siku za Hatari

SIKU HIZO zilikuwa siku za hatari kwa kanisa la Kristo. Injili ikawa imepotea, lakini desturi za kidini zikawa zimeongezeka, na watu wakawa wameleweshwa na kodi za udhalimu. Hawakufunzwa tu juu ya kumwangalia papa kama mpatanishi, bali kutegemea kazi zao kwa msamaha wa dhambi. Misafara mirefu, matendo ya kutubu, ujenzi wa makanisa, na sanduku ya mifupa ya wafu, na madhabahu, malipo ya pesa nyingi kwa kanisa hiyo na mengine yafananayo na hayo matendo yaliunganishwa ili kutuliza hasira ya Mungu au kupata pendekezo lake; kana kwamba Mungu ni kama wanadamu, wa kukasirishwa kwa mambo ya mchezo, au kufanya amani kwa zawadi ama matendo ya toba!

Giza likaonekana likikuwa sana. Kuabudu sanamu ikawa kitu cha kawaida. Mishumaa ikawashwa mbele ya sanamu, na maombi ikatolewa kwa hizo sanamu. Desturi za upuzi na za uchawi zikashinda. Mawazo ya watu yakawa yametawaliwa na mambo ya wachawi hivi kwamba fahamu za watu zikawapotea. Huku makuhani na maskofu walikuwa wenye kupenda anasa, na waharibifu, ingetarajiwa tu ya kwamba watu wanaowangalia hao kwa uongozi nao pia wangezamishwa ndani ya ujinga na uasherati.

### Askofu Mwenye Kiburi

HATUA nyingine ndani ya majivuno ya kipapa ikachukiliwa, ambapo, katika karne ya kumi na moja, Papa Gregory wa saba alitangaza ukamilifu wa Kanisa la Rumi. Kati ya maazimio ambayo alitangaza moja yapo ni ile ya kwamba kanisa halijakosa, na halitaanguka, vile yanavyosema Maandiko. Lakini ushahidi wa Maandiko hauambatani na madai hayo. Askofu huyu mwenye kiburi alidai pia kuwa ana uwezo wa kuondoa wafalme, na kutangaza ya kwamba hakuna yeyote atakayerudisha nyuma maamuzi aliyoyatamka, lakini kwamba anamamlaka yake kuirudisha nyuma maazimio ya wengine wote.

Ni tofauti ya namna gani kati ya kiburi kingi cha huyu askofu mwenye kujiinua na upole na unyenyekefu wa Kristo, ambaye amejiwakilisha Yeye mwenyewe mlangoni pa moyo, ili Yeye apate kuingia na kuleta samaha na amani, na aliyewafunza wanafunzi Wake ya kwamba: "Na mtu ye yote anayekuwa wa kwanza kwenu, na

awe mtumishi wenu". Mathayo 20:27.❑

# GIZA LAENDELEA

KUENDELEA kwa karne nyingi kukashuhudia kuongezeka kwa makosa yaliyotolewa kutoka Rumi. Hata kabla ya kusimamishwa kwa Upapa, mafundisho ya walimu wa kishenzi yalikuwa yamekubalika kwa kuingiza mfuto kanisani. Wengi waliodai kuwa wameogoka pia walikuwa wanaendelea kushikilia mafundisho ya walimu wa kishenzi, na hawakuendelea na mafundisho yake hao wenyewe, waliwasukumia wengine kama njia ya kuendeleza mvuto wao kati ya wasioamini. Makosa makubwa yakaingizwa ndani ya imani ya Wakristo. Ya mbele mbele kati ya hayo ilikuwa ni imani juu ya kutokufa kwa mtu wa asili na yeye kujifahamu akiwa angali amekufa. Fundisho hili likaweka msingi ambao Rumi ilisimamisha mafundisho kuhusu sala za watakatifu na kumuabudu Bikira Mariamu. Ambapo kutokana na hili kukatokea pia uzushi kuhusu kuteketezwa milele kwa wasio tubu, ambao mwanzo yalishirikishwa katika imani ya kipapa.

Basi njia ikaandaliwa kwa kuingizwa kwa uvumbuzi mwingine zaidi wa kanisa la kishenzi, ambaye Rumi iliuita mahali pa ahera, na kufanya kuwa tisho kwa wajinga na umati wa wachawi. Kwa zushi huu ni hakikisho la kuwepo kwa pahali pa kuteke-tezwa, ambapo roho za wale ambao hawajapata laana ya milele wangepata mateso kwa ajili ya dhambi zao, na kutokana hapo, wanapo wekwa huru kutoka kwa uchafu wao, huruhusiwa kuenda mbinguni.



### *Mali ya Ujanja*

NA TENA uvumbizi mwingine ungelihitajika ili kuiwezesha Rumi kujipatia faida kutoka na hofu na ufisadi wa waumini wake. Hili pia lilichangiwa kutokana na fundisho la kujifurahisha. Ondoleo la dhambi kamili, zilizopita, na za leo, na hata wakati ujao, na kufunguliwa kwa maumivu yote yaliahidiwa, kwa wale wote wangejiorodhesha katika vita vya askofu katika kueneza milki yake ya muda, kwa kuwatesa maadui zake, au kuwafutilia mbali maadui wake wa kidini. Watu pia walifunza ya kwamba kwa malipo ya pesa kwa kanisa wangejifungua wen-yewe kutoka dhambini, na pia kuwafungua roho za marafiki zao waliokufa ambao wamefungwa ndani ya moto uwakao. Kwa pesa hizo Rumi ikajijazia masanduku na ikadumisha ufahari, anasa, na ufisadi wa wale waakilishi wa yule asiyekuwa na mahali pa kuweka kichwa chake.

> **"Papa si mwakilishi tu wa kristo yesu, bali ni yesu kristo aliyefichwa ndani ya vazi la mwili."** *The Catholic National* Julai, 1895.

### *Muumbaji Aliumba*

AGIZO LA maandiko kuhusu Pasaka ya Bwana lilikuwa limebadilishwa kwa kafara ya miungu ya Misa. Makuhani wa Ki-papa wakijifanya, kwa manongonezo yao ya bure, ili kuugeuza mkate wa kawaida na divai kuwa "mwili na damu asili ya Kristo"- Kadinali Wiseman, "Hali Halisi ya Mwili na Damu ya Bwana Wetu Yesu Kristo katika Ushirika Mta-katifu wa Kikristo, Inaothibitishwa Kwa Maandiko," hotuba ya 8, sehemu ya. 3, fungu la. 26. Pamoja na kiburi cha makufuru, wakatangaza wazi kuwa na uwezo wa kumuumba Mungu, Muumbaji wa vitu vyote. Wakristo walihitajika, kwa maumivu ya kifo, kukiri imani yao kwa huu uzushi wa kuogofya, wa matukano kwa Mbin-guni. Wengi wa watu waliokataa walitupwa kwa moto.

### *Mamilion ya Waliouwawa*

KATIKA karne ya kumi na tatu ndipo kuliposimamishwa kile chombo cha ajabu cha Kipapa-yaani baraza kuu la kuhukumia wazushi wa dini. Mfalme wa giza alitenda kazi pamoja na viongozi wa serikali ya kipapa. Katika baraza yao ya siri Shetani na malaika wake walitawala mawazo ya watu waovu, huku malaika wa Mungu walisimama katikati yao bila kuonekana, wakichukua habari za kutisha za uwekaji nguvu sheria yao ovu na pia wakiandika historia ya kutisha sana machoni pa wanadamu. Makundi ya waliouwawa wanamlilia Mungu kuwalipizia kizazi juu ya utawala huo wa kuasi.

> **"Papa Yohana wa pili aliomba msamaha kwa vita kati ya wakatoliki na waprotestanti kule ulaya wakati wa kuzuia matengenezo".** *Habari kutoka marekani na habari za ulimwengu* Julai 3, 1995.
>
> Hii na habari zingine kama hizi na stakabadhi ya maungamo yasionyooka kwa jukumu la mamilioni ya wafia dini wakati ule wa zama za giza. Bibilia inatabiri kuwa katika nyakati za taabu zilizo mbele yetu, upapa na wafuasi wake watakibilia tena nguvu za serikali ili wawazuie wasiok-ubaliana nao.

### *Giza Totoro*

MAFUNDISHO ya kipapa yalikuwa ya udhalimu kwa ulimwegu. Wafalme na wenye mamlaka walikuwa wanatii sheria za askofu wa Kirumi. Maisha ya watu, wakati huo na umilele, yalionekana kuwa chini ya utawala wake. Kwa mamia ya miaka mafundisho ya Kirumi yameenea sana na kupokelewa bila swali, kanuni zake zimeadhimishwa na wote. Na wenye mamlaka Kani-sani wamesaidiwa kwa ukarimu. Tangu zamani Kanisa la Kirumi halikuwa limefikia kiwango cha heshima ya juu, fahari, au uwezo kama huu.

### *Maovu Yasiozuilika*

LAKINI "Adhuhuri ya Kipapa ilikuwa usiku wa manane wa ulimwengu."- J.A. Wylie, Historia wa Waprotestanti, book 1, ukurasa wa 4. Maandiko Matakatifu yalikuwa karibu kutojulikana, sio tu kwa watu, bali kwa makuhani pia. Kama Wafarisao wazamani, viongozi wa Kipapa walichukia nuru ambayo ingeonyesha dhambi zao. Sheria za Mungu, ambazo ni kipimo cha haki, baada ya kuodolewa, ndipo walipotumia nguvu bila kikomo, na kufanya mambo ya ufisadi bila kizuizi. Udanganyifu, tamaa, na mambo ya usherati zikashinda. Watu hawakujitenga katika kila tendo la uhalifu ambalo lingewaletea utajiri au madaraka. Majumba ya askofu na upapa yalikuwa na matendo ya upotovu ya usherati. Baadhi ya maaskofu waliokuwa wanatawala walikuwa na hatia ya uhalifu wa kuchukiza hata viongozi wa serikali wabaya sana wasioweza kuvumiliwa. Kwa muda wa karne nyingi Ulaya haikufanya maendeleo katika elimu, ufundi, au utamaduni. Kudhoofika kimwili na kimawazo ilikuwa imeanguka juu ya ulimwengu wa Wakristo.

### *Wageuzi wa Mafundisho Wakataa*

KWA KUKOSEKANA kwa hekima ya Neno la Mungu ndiyo sababu iliyoruhusu Upapa kuta-wala ulimwengu katika Zama za Giza. Karibu mwisho mwisho wa zama hizo, jinsi ufahamu wa Neno la Mungu ulianza kufunuka, watu walianza kuyapinga maovu yalioenena katika nyakati hizo. Hao Wageuzi Waprotestanti walirushia mbali pingu za maovu na uchawi yalionekana

> **"Kwa kukiri imani iliyo kinyume na kanisa la kirumi, historia inanakili watu zaidi ya milion moja waliouwawa"** *Muhtasari ya masomo ya Bibilia*, ukurasa a 16.
>
> **"Katika agosti 24, 1527 wakatoliki wa kirumi katika ufaranza, kupitia kwa mpango uliotengenezwa chini ya wanaojiita kuwa ni wa familia ya kristo, wakawaua wakristo wasiokubaliana na mafundisho ya kirumi elfu sabini, kwa muda wa miezi miwili. Na papa akafurahi aliposikia habari ya matokeo."** *Western Watchman*, Nov. 21, 1912, (Catholic).

wakati huo, na wakaanza kuruhusu nuru ya Neno la Mungu kuangaza. Watu Hawa wakapokea jina la kuitwa wanaojitenga, sababu, walipouelewa ukweli wa Neno la Mungu waliona kuwa ni lazima wakatae na kupinga maasi ya Kikatoliki kama wengekuwa waminifu kwa Mungu. Kwa mara nyingine tena katika historia ya sayari hii maarifa ya Neno la Mungu yalikuwa yamesahaulika. Linganisha ufahamu Wageuzi wa mafundisho kwa Upapa na imani ya kizazi hiki cha wakati huu.

### *Mafundisho ya Kipapa Yakataliwa*

MARTIN LUTHER alisema, "Najua kuwa papa ni Mpinga Kristo, na ya kwamba kiti chake ni kile cha ya Shetani mwenyewe. Utawala wa Kipapa ni msako wa wote, ambao umeamuriwa na askofu wa Kirumi, kwa kusudi la kushusha na kuangamiza roho za watu."

Charles Spurgeon alisema, "Ni lazima tuwaonye kwa ushujaa wenye busara wale wanaojielekeza kwa madanganyifu ya Rumi; ni lazima tuwaambie juu ya matendo ya giza ya Upapa."

John Knox alisema papa ni "mpinga kristo halisi."

John Wesley alisema juu ya Upapa kuwa, "bila shaka, yeye ni Mtu wa Kuasi, kwa vile anavyoongeza kila aina ya dhambi bila kiwango."

John Calvin alisema, "Tuna-mwita papa wa Kirumi Mpinga Kristo."

### *Waprotestanti Wasahau Yaliopita*

HIVI LEO wazao wa watakatifu walioifia dini wamesahau ni kwa nini wanajiita Waprotestani. Tazama ya fuatayo:

"Sasa ni wakati kwa Waprot-estani kumwendea mchungaji (papa) na waseme, 'Tutafanya nini ili tuje nyumbani?' " Dr. Robert Schuller, alisema *Los Angeles Herald Examiner*, Septemba 19, 1987.

"Mkuu wa Waprotestanti katika Marekani na makanisa ya ki Otho-dox ya Mashariki ambaye walikuwa wanakutana na Papa Yohana Paulo II katika siku ya Ijumaa alipongeza maongeo yao ya kwanza ya mashauriano mengi kuwa nguzo katita njia ya umoja mkuu.... Mchungaji Donald Jones, wa kanisa la wafuasi wa Kanisa la Kimethodisto na ndiye mwenye kiti wa idara ya mafundisho ya kidini katika Chuo Kikuu ya Carolina Kusini, aliutaja makutano huo kuwa, "ni mkutano wa umoja tena wa maana na wa muhimu katika karne hii."... Mchungaji Paul A. Crow Jr., wa Indianapoli, msimamizi mkuu wa Kanisa la Wakristo (Wanafunzi wa Kristo), naye aliutaja kuwa ni 'siku mpya katika kuungana pamoja' kwa kufungua nyakati za mbele ambazo Mungu 'anatusukuma kwa pamoja.' " *Mshauri wa Montgomery*, Sebtemba. 12, 1987.

"Ikiwa mafundisho ya Kikatoliki Itaendelea kuwa katoliki halisi katika siku sijazo, ambazo ninazo zitarajia chini ya papa wa wakati wa sasa, ndipo tofauti za kitheologia Itakuwa, ni udanganiyifu, lakini mapatano yetu na wakatoliki juu ya utamaduni wa serikali itakuwa na kina kirefu." David Wells, *Eternity Magazine*, Septemba 1987.

"Mafundisho ya Wakatoliki na Waprotestanti kuhusu maisha ya Ukristo inafanana. Je sio ya maana kwa wakristo wa badaye?" J. I. Packer, *Ukristo wa Sasa*, Juni 22, 1992.

Waprotestanti wamepoteza asili yake. Iliteuliwa kupinga na kushutumu makosa ya Rumi. Lakini yuko tayari sasa kukumbatia sasa. Wakati ulimwengu shambulizi ya mwisho ya Rumi, maadui wa zamani wanaunda urafiki. Ulimwengu wa Waprotestanti wamesahau ya kwamba wana-husika katika vita ya umilele, na kwa sababu ya kupenda kupoteza maarifa, imekusudiwa kuang-amizwa.❑

# SHERIA NA MPANGO NDIO JARIBU KAMILI

TANGU HAPO mwanzo wa vita kuu huko mbinguni imekuwa ni kusudi la Shetani kuangusha sheria za Mungu. Kudan-ganya watu, na kwa kuwaongoza kuvunja sheria za Mungu, ndio lengo ambalo amefuatilia kwa mathubuti sana. Iwe ni kwa kutekelezwa kwa kuondoa sheria ya Mungu kabisa, au kupuuza mmoja ya maagizo yake, matokeo itakuwa sawa mwishowe. Anayejik-waa katika "Sehemu moja" huony-esha madharau kwa jumla ya sheria; mfuto wake na kielelezo chake katika upande wa kuasi; anakuwa "mkosaji juu ya yote". Yakobo 2:10. Kwa kujaribu kutia madharau kugeuza mafundisho ya bibilia, na makosa imefundishwa ndani ya imani ya maelfu wanaokiri kuwa wanaamini maandiko. Pambano kuu la mwisho kati ya ukweli na uongo ndiyo mashindano ya mwisho ya vita vya miaka mingi juu sheria za mungu. Juu ya mapigano haya ndiyo tunaingia sasa mapigano kati ya sheria za watu na maagizo ya mungu, kati ya dini ya Biblia na dini ya uongo na mafundisho ya wanadamu.

Ukafiri umeenea katika kiwango cha juu, sio katika ulimwengu hasa bali ndani ya kanisa. Wengi wamefikia kukataa mafundisho ambayo ni msingi hasa wa imani ya wakristo, ukweli thabiti uumbaji jinsi inavyotolewa na wanaoongozwa na roho mtakatifu, kuanguka kwa mwanadamu, upatanisho, na kuwako mileie ya sheria za mungu, ndiyo inakataliwa kwa wazi, iwe ni kwa yote au sehemu, na umati mkubwa wanaokiri kuwa wakristo katika ulimwenguni. Wachungaji wengi wanawafundisha watu wao, mwalimu mkuu na walimu wa chini wanawafundisha wanafunzi wao, kuwa sheria za mungu zimebadilishwa au kutenguliwa; na wale wanaoangalia masharti yake kuwa ni ya muhimu, na ya maana kutii, ndiyo wanafikiriwa kuwa wanafaa kudhihakiwa na kudharauliwa.

### *Kufanya Sanamu ya Mufundisho*

KWA KUKATAA ukweli, watu wan-amkataa mwanzilishi wake. Kwa kukanyangia chini sheria za Mungu, wanaukataa uwezo wa mtoa sheria. Ni rahisi kutengeneza sanamu ya mafundisho ya uongo na mambo ya kubahatisha kama vile kuchonga sanamu ya miti au mawe. Kwa kusingizia vibaya juu ya tabia ya mungu, shetani huongoza watu kumwona yeye katika tabia mbaya na wengi sanamu ya elimu imetawazwa katika mahali pa mungu; Huku mungu aishie jinsi amefunuliwa katika neno lake, ndani ya Kristo, na katika kazi ya uumbaji, anaabudiwa lakini na wachache. Maelfu wanaheshimu Maumbile huku wakikana mungu wa maumbile. Ingawa ni kwa umbo tofauti, uabuduaji wa sanamu zimo katika ulimwengu wa wakristo sasa kama vile zilimo kuwamo katikati ya waisraeli katika wakati wa Elija miungu ya watu wengi wanaokiri kuwa ni werevu, wa walimu, ya watunga mashairi, ya wanasiasa, ya waandishi wa habari miungu ya majumba mengi mazuri ya vyama vingi na vyuo vikuu hata na baadhi ya majumba ya walimu bora ni kidogo kuliko baal, mungu jua ya wafoenike.

Hakuna uongo hasa unaokubaliwa na ulimengu wa wakristo wanayogonga kwa ufasiri juu ya sheria za mungu hakuna yanayapinga zaidi yale yanayonenwa, hakuna yalio na matokeo mabaya kuliko mafundisho ya kisasa, yanayo chukua nafasi kwa haraka sana kiasi kwamba sheria za mungu hazina masharti juu ya watu. Iwapo kama wachungaji wanao julikana, wangehubiri kwa wazi kuwa sheria inaoongoza nchi yao na kutunza haki za wazalendo Sio ya lazima-ya kwamba zinazuia uhuru wa watu, na kwa hivyo hazifai kuzitii, ni kwa muda gani watu hawa wangevumiliwa katika jukwaa? lakini



ni jambo mbaya kupuuza sheria za serikali na nchi kuliko kukanyangia chini maagizo ya mungu ambayo ni misingi wa Serikali zote?

### Dhambi Kukosa Kuwa Dhambi

POPOTE maagizo ya mbinguni yanakataliwa, dhambi huonekana si dhambi tena ,na haki ya mungu haipendwi. wale wana-okataa kunyenyekea kwa serikali ya mbinguni hao hawapaswi kujitawala wenyewe. kupitia kwa mafudisho mabaya roho wa ukaidi huwa amepadwa kwa watoto na vijana, ambao katika uasi wao hawawezi kujizuia, na kuvunja sheria na jamii ya uzinifu ni matokeo yake. huku wakidhihaki imani ya wale wanaotii maagizo ya mungu, umati wa watu hupendelea kukubali madanganyo ya shetani. wanatawaliwa na tamaa na kuendelea kufanya dhambi ambazo zinaleta hukumu za mungu kwa mataifa.

### Jamii Katika Machafuko

TAYARI mafundisho ya watu kufuguliwa kutoka kuyatii maagizo ya mungu, fundisho hili limepunguza nguvu za wengi kutoka masharti hayo na kufungua milango ya uasi ulimwenguni. Uvunjaji wa sheria, ufisadi na machafuko mengi yanaendelea kuingia ndani yetu kama maji mengi. katika jamii, shetani anafanya kazi. Bendera yake hupepea hata katika jamii ya wakristo. kuna chuki, masengenyo, unafiki, faraka, wivu, vita, kusalitiana, na kujitoa kwa anasa. muungano wote wa sheria na mafundisho ya kidini, ambao ungefanya msingi mwema wa maisha ya umoja, sasa waonekana kuwa ni fungu linalotikisika likiwa tayari kuanguka kwa uangamizi. Wakaidi wale wabaya, wanapotupwa gere-zani kwa makosa yao, mara nyingi huonekana kupewa zawadi na kupokelewa vizuri kana kwamba wamepata jina nzuri la kutamanika. tabia yao na uovu hutangaza hadharani. Waandishi wa habari huchapisha uasi wa kuchukiza, hivi wakishawishi wengine kufanya ujanja, wizi na uaji, na shetani hujiinua kwa ushindi wa njia ya kishetani. ufisadi, tamaa ya kumwaga damu, kuongezeka kwa hali ya juu ya tamaa,haya yote yanapasa kuwaamsha wote wamchao mungu,




kuuliza ni nini kitafanywa ili kuzuia mafuriko ya uovu.

### Sasa Maandiko Yakataliwa

UASI NA giza la kiroho vilivyo pata ushindi chini ya utawala wa kirumi, yalikuwa ni matokeo yasio epukika Rumi kugandamiza chini maandiko matakatifu, na ni wapi tutapata sababu ya kuenea kwa ukatili, kukataa sheria ya Mungu, na matokeo ya machafuko, chini ya mwangaza mkubwa wa injili katika kizazi kilicho na uhuru wa ibada? Kwa shetani hawezi tena kuiweka dunia chini ya utawala wake kwa kukanyagia chini maandiko, sasa atatafuta njia zingine ili kutekeleza lile kuzudi lake. kwa kuitoa imani katika bibilia, hili hutekeleza kuzudi lake kama vile tu kuiharibu bibilia yenyewe. Kwa yeye kufundisha ya kwamba,sheria ya mungu haidumu tena, amefaulu kuwaongoza watu kuifunja sheria kana kwamba hawakujua kabisa maagizo yake. Na sasa kama zile za kwanza, yeye hufanya kazi kupitia kwa kanisa ili kuendeleza matakwa yake. Muungano wa madhehebu ya wakati huu, wamekataa kuisikiza kweli isiojulikana na ambayo imefunuliwa wazi katika maandiko, na kwa Kushindana na hayo maandiko, wamejitafutia tafsiri zao na kuchukuwa sehemu ambayo imepanda kote mbegu za tashwishi.

Kwa Kuendelea kushikilia madanganyo ya upapa juu ya kutokufa kwa mwenye dhambi, na hali ya mtu wakati amekufa, wameikataa kinga ya pekee dhidi ya madanganyo ya mizimu. Fundisho juu ya kuteswa milele limewaongoza watu wengi kutoiamini biblia. Na jinsi vile madai ya sheria ya nne imesisitizwa kwa watu, imepatikana ya kwamba imefunganishwa kwa kuitunza Sabato ya siku ya saba; na kwa njia yao ya kipekee ya kujiepusha na majukumu ambayo hawataki kutekeleza, hao walimu wenye sifa, hutangaza kwamba, sheria ya Mungu haimo tena. Kwa hivyo wametupilia mbali sheria na Sabato vyote pamoja. Jinzi matengenezo ya Sabato yanaendelea, kukataa huku kwa sheria za Mungu ili kuepuka madai ya sheria ya nne kutaendelea sana ulimwenguni.❑

# ZAMA ZA GIZA ZITARUDIWA

UJANJA WA shetani katika vita vya mwisho na watu wa Mungu ni sawa tu na ule alioutumia katika mwanzo wa vita kuu kule mbinguni. Alidai ya kwamba alitafuta kuiinua serikali ya mbinguni, huku kisiri alikuwa akitafuta njia za kuiangusha. Na kazi ile ile tu aliokusudia kukamilisha, aliwawekea malaika watakatifu. Ujanja kama huo wa udanganyifu umeonekana katika historia ya kanisa la kirumi. kanisa hili limekuwa likidai ya kuwa ni mwakilishi wa mungu wa mbinguni, huku likitafuta sana kujiinua juu ya mungu, na kubadilisha sheria zake. Chini ya utawala wa kirumi, wale waliouwawa kwa utiifu katika injili, walikataliwa kuwa ni watenda mabaya, wakasemewa kuwa wam-eshikana na shetani, na kwa kila njia iwezekanavyo walitafutiwa kufunikwa na aibu, ili kuwafanya waonekane machoni pa watu na hata machoni pao wenyewe kuonekana kuwa wakaidi wakubwa. kwa hivyo ndivyo tu itakavyokuwa hivi sasa. huku shetani akitafuta kuwaa-ngamiza wale wanaoshika sheria ya mungu, atawafanya washitakiwe kuwa wavunja sheria, na kama watu wasio mheshimu mungu na wanaoleta hukumu za mungu duniani.

### Kushurutisha Kwa Ukatili

MUNGU hajawahi kulazimisha nia ya mtu au dhamira, lakini njia ya shetani mara nyingi, ili kuwatawala wale ambao hawawezi akawadanganya hulazimisha kwa ukatili. kupitia kwa hofu ama lasimisho, hujitahidi kutawala dhamira na kujiletea heshima kwake mwenyewe.ili kutekeleza jambo hili,yeye hufanya kazi yake kupitia kwa uwezo wa kidini na wa kiserikali, akiwasukumia kuiweka sheria ya binadamu kupingana na sheria ya mungu.

Wale wanaoiheshimu sabato ya Bibilia,watakataliwa kuwa maadui wa sheria na mpango, wanaovunja mahusiano na jamii, wanaleta machafuko na uchochezi, na kuleta hukumu za mungu duniani. Msimamo wa yale yalio katika dhamira zao, utatan-gazwa kuwa ukaidi, utukutu na kudharau mamlaka. Watatukanwa kuwa hawana upendo kwa serikali. Wachungaji wale wanaokataa masharti ya sheria ya mbinguni, wataongea kutoka kwa masinagogi, hukumu ya kila mmoja kunyenyekea kwa utawala wa serikali kuwa umechaguliwa na mungu. Katika majumba ya sheria ya kutoa hukumu, wale wanazishika sheria za mungu wataongewa vibaya na kudharauliwa. Mambo ya uongo yatawekewa juu ya maneno yao na katika nia zao watawekewa mambo ma-baya.

### Nuru Itabadilishwa Kuwa Giza

KAMA VILE makanisa ya kiprotestanti yanakataa mafundisho wazi ya Bibilia yanayotetea sheria za mungu; watatafuta sana kuwanyamazisha wale ambao hawawezi kuw-adanganya kwa Bibilia. licha ya hawa kujipofisha kwa ukweli kabisa, sasa wachukua njia itakayowaongoza kuwatesa wale wanaokataa kufanya yale ambayo ulimwengu wa kikristo wanatenda, kwa kuku-bali sabato ya kipapa

### Kunyimwa Uhuru Wa Dhamira

VIONGOZI wa kanisa na serikali wataungana pamoja kwa kuhonga, kushawishi au kuwalazimisha watu wa viwango vyote kuiheshimu Jumapili. Kwa kukosa sheria za mbinguni, kutabadilishwa na sheria za kimabavu. Machafuko ya

# SHETANI, MPANDA MAOVU, ALITOKA WAPI?

### *Mwanzo wa Dhambi*

KWA MAWANZO ya wengi, mwanzo wa dhambi na sababu yake kuendelea ni chanzo cha wasiwasi mkuu.

Wanaona kazi ya uovu ni matokeo yake ya kutisha huzuni na wanauliza ni vipi haya yote yaweza kuwepo chini ya uongozi wa yule mtakatifu aliye na hekima ya mbinguni, uwezo na upendo. Ni vigumu sana kueleza mwanzo wa dhambi ili kutoa sababu ya kuwepo kwake. Na zaidi ya hayo yaweza kueleweka kuhusu mwanzo wa dhambi na mwisho ili kuweka wazi haki na wema wa Mungu katika kujulikana hali ya maoni. Dhambi ni mdukizi, ambaye kuonekana kwake hakuna sababu ya kutoa. Kama kungelikuwa na kisingizio cha kuwepo, kwake ama sababu ya kuendendelea kuwepo kwake, basi ingekoma kutokuwa dhambi.Maelezo yetu kuhusu dhambi ni yale tu yametolewa katika neno la Mungu. Ni "Uvunjanji wa sheria."

### *Upendo wa Mungu na Kiburi*

SHERIA ya upendo ikiwa ni msingi wa serikali ya Mungu, furaha ya viumbe vyote ilitegemea umoja mkamilifu pamoja na maagizo yake ya haki. Mungu hutumainia kutoka kwa viumbe vyake huduma ya upendo na unyenyekevu unaotokana na kufurahia tabia yake. Mungu hafurahishwi na Mapatano ya kulazimishwa, na kwa wote huwapa uhuru kuna mmoja tu aliyechagua kupofusha uhuru huu. Dhambi ilianzishwa na yeye, ambaye alikuwa karibu sana na kristo, na alikuwa ameheshimiwa sana na Mungu na ndiye aliyesimama juu ya mamlaka na utukufu kati ya wenyeji wa mbinguni. Kabla ya kuanguka kwake, Nyota ya asubuhi alikuwa kerubi wa kwanza afunikaye, takatifu na isionajizi. tazama Ezekieli 28:12-15.

Huyu nyota ya asubuhi angeendelea kuwa na pendekezo na Mungu, kupendwa na kuheshimiwa na jeshi lote la malaika, akiuonyesha uwezo wake kwa kuwabariki wengine na kumtukuza muumba wake. Lakini nabii asema hivi " Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako, umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako." Ezekiali 28:17. Kidogo Kidogo huyu nyota wa asubuhi akaja kutamani kujiinua nafsi yake."Nawe ulisena nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu. Nami nitaketi juu mlima wa makutano....nitapaa kupita vimo vya mawingu: nitafanana na yeye aliye juu! Isaya 14:13-14. Badala ya kutafuta kumfanya Mungu kuwa mkuu katika upendo na umoja kati ya viumbe zake, ili Juhudi za yule nyota ya asubuhi kujitakia huduma na heshima kutoka kwa wale malaika. Na kwa kutamani heshima ambayo Mungu wa milele alikuwa amempa mwanawe huyu mkuu wa malaika akatamania nguvu ambazo zilikuwa ni za kristo peke yake.

Mwana wa Mungu ndiye aliyejulikana kuwa mwenye mamlaka mbinguni, aliyekuwa na uwezo na mamlaka sawa na Baba yake. Katika baraza zote za Mungu, kristo alikuwa ni mshiriki, huku shetani hakuruhusiwa kuingia katika makusudi ya Mungu. "kwa nini huyu malaika mkuu akauliza "Kristo aweza kuwa na utawala? Kwa nini yeye anaheshimiwa kuliko yule nyota ya Asubuhi.

### *Kufunikwa na siri*

SHETANI alikuwa ameheshimiwa sana, na matendo yake yote yalikuwa yamefunikwa na siri. Hivi kwamba ilikuwa ni vigumu kufunua kwa malaika asili ya kweli ya kazi yake. Mpaka wakati ule tabia yake ilionekana vizuri, dhambi haingeonekana kuwa mbaya jinsi ilivyo-kuwa, kwa hivyo haikuwa imepata mahali katika ulimwengu wa Mungu, na hakuna viumbe watakatifu waliokuwa na wazo juu ya uasi na udanganjifu wake. Haw-angetambua matokeo ya kutisha, ambayo yangetokea kwa kuiweka kando sheria za Mungu. Kwa Mungu kuichukulia dhambi, angetumia haki na kweli Shetani angetumia kile ambacho Mungu hangetumia..... kushawishi na udanganyifu. Mate-ngano ambayo yalisababishwa na kazi yake mbinguni, shetani aliwekelea juu sheria na serikali ya Mungu. Maovu yote alidai kuwa ni matokeo ya uongozi mbaya wa Mungu. Alisema kuwa ilikuwa ni kuzudi lake kurekebisha maagizo ya Mungu. Kwa hiyo ilikuwa muhimu ili apate kuonyesha asili ya madai yake, na kuonyesha mabadiliko yake katika sheria za Mungu. Kazi yake mwenyewe ni lazima imuhusu yeye mwenyewe. Shetani alidai tangu hapo mwanzo yakwamba hakuwa muasi. Ni mpaka angekuwa na muda wa kujionyesha katika maovu yake. Ulimwengu mzima ni mpaka wangemuona mdanganyifu huyu akifunuliwa.

### *Roho Yule Yule*

ROHO YULE yule aliyesukumia uasi mbinguni bado anachochea uasi hapa duniani shetani ameendelesha pamoja na wana-damu ujaja ule ule alioutumia pamoja na malaika. Kwa kukosoa tabia ya Mungu kama jinzi alivyo fanya huko mbinguni, kwa kumfanya yeye kuwa mkali na mdhalimu Shetani akamdanganya mwanadamu kufanya dhambi. Na alipofaulu sana kwa umbali, akat-angaza kuwa masharti ya Mungu yasio ya kweli yalimfanya mwan-adamu kuanguka, kama jinsi maagizo hayo yaliongoza kuanguka kwake Mungu alitoa ushahidi kwa upendo wake kwa kumtoa mwana wake wa kipekee kufa kwa ajili ya kizazi kilichoanguka. Katika upat-anisho tabia ya Mungu hufunuliwa. Mabishano makuu ya msalaba huudhihirishia ulimwengu wote ya kwamba matokeo ya dhambi ambayo yule nyota ya Asubuhi alikuwa amechagua hayakuwa kwa njia



yoyote lawama juu ya serikali ya Mungu.

### *Zaidi ya Wokovu*

HAIKUWA tu kwa kukamilisha wokovu wa mwanadamu ili kristo akaja duniani kuteseka na hata kufa. Alikuja "kuipanua" sheria na "kuitukuza" sio tu wenyeji wa ulimwengu huu wanaohitajika kutunza sheria jinsi inayohitajika, lakini ilikuwa ni kudhihirisha nchi zote za mbinguni ya kwaba sheria za Mungu hazibadiliki. Kama madaiyake yangewekwa kando, basi mwana wa Mungu hangehitajika kujitoa maisha yake kuwa patanisha wenye dhambi. Kifo cha kristo huhakikisha kuwa sheria za Mungu hazibadiliki.

Katika siku ya mwisho ya hukumu itaonekana ya kuwamba hakuna sababu ya dhambi kwendelea msalaba wa kalwari, huku ukitangaza ya kwamba sheria haibadiliki, huitangazia mbinguni kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. Katika kilio cha mwisho cha mwokozi "imekwisha" onyo la mauti la shetani likalia. Vita kuu vilivyokuwa vimeendelea kwa muda mrefu basi hapo vikaamuliwa, na kuondolewa milele kwa maovu kukahakishiwa. Ulimwengu wote ungekwa mashahidi kwa asili na matokeo ya dhambi.❑



kisiasa yanaendelea kuharibu upendo wa haki na wa kuipenda ile kweli ya Bibilia, ili kupata sifa kwa watu, watajishusha kwa hitaji la wengi la kulazimisha kutunza Jumapili. Uhuru wa dhamira ambao umegharimu kujitoa sana hautaendelea kuheshimiwa tena. Katika vita inayokuja mbele yetu, hutaona utimilifu wa maneno ya nabii: "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu." Ufunuo 12:17.

Bali na wale wanaozishika amri za Mungu na Kuwa na imani ya Yesu, malaika wa tatu analenga kundi lingine ambalo limepewa onyo la kutisha kuhusu makosa yao, Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, mtu awaye yote akimsujudu huyu mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake." Ufunuo 14:9-10. Tafsiri halisi ya mifano ambayo imeonyeshwa hapa, ni ya muhimu sana kwa kuelewa ujumbe huu. Ni nini hasa kinaakilishwa na mnyama, sanamu na alama yake?

**Wale ambao wanaiheshimu Sabato ya Bibilia watashutumiwa kuwa maadui wa sheria na mpango.**

# Kutafsiri Mifano

## Yule Mnyama

MSTARI WA unabii ambapo mifano hii inaweza kupatikana inaanza na Ufunuo 12, na yule joka alitafuta kumwa-nga-miza Kristo katika kuzaliwa kwake. Joka anasemwa kuwa ni shetani (Ufunuo 12:9); yeye ndiye yule aliye msukuma Herode kumtafuta kumuua Kristo. Lakini mwakilishi mkuu wa yule shetani kwa kufanya vita dhidi ya Kristo na watu wake katika karne zile za kwanza za imani ya Waristo ilikuwa ni enzi ya Kirumi, ambapo dini ya kishenzi ndiyo iliyotawala. Basi, huku joka mwanzoni akimwakilisha Shetani, ni, nyumaye, alikuwa mfano wa Rumi ya kishenzi.

## Mnyama Mwenye Mfano wa Chui

KATIKA sura ya 13 (fungu la 1-10) imeonyeshwa mnyama mwingine, "Aliye na mfano wa chui". Ambaye kwa huyo mnyama - Shetani na rumi ya kishenzi - walimpa " nguvu zake na kiti chake na uwezo wake." Mnyama huyu anayefanana chui, Jinzi waprotestanti wengi wanaamini huakilisha upapa, ambao ulipata nguvu kiti na mamlaka ambayo hapo mwanzo yalishikiliwa na enzi ya zamani ya kirumi. Kwa mnyama huyu anayefanana kama chui inase-mwa ya kwamba. "Naye akapewa kinywa chake amtukane Mungu na kulitukana jina lake na maskani yake, hao wakaao mbinguni." Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa, "Unabii huu ambao karibu kufanana sana na maelezo ya pembe ndogo katika Danieli 7. Bila swali hii hulenga upapa." Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili." Na nabii ana sema, nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti." Na tena: "Mtu akiua kwa upanga atauawa kwa upanga" ufunuo 13:10. miezi arobaini na miwili ni sawa na" wakati nyakati mbili na nusu wakati "miaka mitatu na nusu" au siku 1260, ya Danieli 7. nyakati ambazo utawala wa kipapa ungegandamiza watu wa Mungu. Kipindi hiki kilianzia wakati wa utawala wa kipapa, mwaka wa 538 A.D, na kumali zikia katika mwaka wa 1798 A.D. Wakati huo papa alichukuliwa mateka na wanajeshi wa ufaranza, utawala wa kipapa ukapata jeraha la mauti, na unabii ukatimika. Mtu akichukuwa mateka, atachukuliwa mateka" Ufunuo 13:10.

## Marekani Katika Unabii

HADI HAPA mfano mwingine unatolewa. Nabii asema, "kisha nikaona mnyama mwingine akipanda juu kutoka katika nchi naye alikuwa na pembe mbili" fungu la 11. Kwa kuonekana kwa huyu mnyama na kuinuka kwake huonyesha kuwa yeye ni tofauti na wale wengine walioonyeshwa katika mifano. Falme kubwa nne ambazo zimetawala ulimwengu zilionyeshwa kwa nabii Danieli kama wanyama wa kuwinda walioinuka wakati pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu juu ya



bahari kubwa. Danieli 7:2 katika ufunuo17 malaika anaeleza kuwa maji yanaakilisha "watu na makutano, na taifa, na lugha. Ufunuo 17:15. Pepo ni mfano wa machafuko. Pepo nne za mbinguni zilizovuma juu ya bahari kubwa huakilisha matukio ya kutisha ya mapinduzi na mageuzi ambayo wafalme wamejipatia utawala.

## Kutoka Katika Nchi

LAKINI mnyama aliye na pembe kama za mwana kondoo alione kana "akipanda juu kutoka katika nchi" Ufunuo 13:11. Badala ya kuangusha falme zingine ili kujipatia mamlaka, taifa linaloakilishwa na huyo mnyama ni lazima litokee katika nchi ambayo

**"Uhuru wa miungu ambayo ime garimu sana, kwa kujitolea haita heshimiwa tena."**

haijawahi kukaliwa tangu zamani, na likuwe pole pole na kwa amani. Basi, halingejitokesha katikati ya msongamano na mataifa ya kufutana. Ya ulimwengu wa zamani yaani mchafuko wa bahari "watu na umati, na mataifa na lugha." Ni sharti lingepatikana katika nchi za magharibi.Ni taifa lipi katika ulimwengu mpya lilikuwa likiinuka kwa nguvu katika mwaka wa 1798, likitoa ahadi za nguvu na ukuu na kuyafuta mawazo ya ulimwengu? Maana ya mfano huu unaingia bila swali lolote. Taifa moja, na ni moja tu linaloshikamana na unabii huu, bila wasiwasi hulenga nchi ya marekani. Tena na tena, wazo sawa na maneno kamili ya mwandishi wa Bibilia yametumiwa na waandishi wa historia kwa kueleza kuinuka na kukua kwa taifa hili. Mwandishi hodari akieleza kuinuka kwa nchi ya marekani anasema "siri ya kuinuka kwake kutoka faragani" na anasema "kama mbegu kimya tuliinuka mpaka kuwa serikali" G.A.Townsend. The new world compared to the old, kurasa 462. Mwandishi wa habari kutoka

**"Ikiwa basi kanisa la katoliki pia linadai haki ya kutofumilia kuhusu mafundisho yake, sio halali kulishutumu kwa kutumia haki hizo. Linachukulia kanuni zisizoweza kufumiliwa sio kama Jukumu takatifu. Kulingana na Warumi 8:11, mamlaka ya serikali yana haki ya kuadhibu hasa waalivu wabaya na kifo baadaye " wazushi" nao pia sio tu kutengwa bali pia kuuawa."** *The Caholic Encyclopedia*, 1911, edition, wi 14, page 766, 768.

**"Ukuta wa utengo kati ya kanisa na serikali ni mfano ambao umejengwa katika historia mbaya, mfano ambao umeonekana kuwa bure kama uongozi wa uamuzi."** Jaji mkuu William Rehnguist, *Jarida la Nyakati*, Desemba 9, 1991.

**Kiongozi wa hivi karibuni wa mahakama kuu ya merikani alitangaza kuwa wakati haki za kidini zinapogongana na mahitaji ya serikali katika katibu moja, mahakama itakuwa upande wa serikali."** *Los Angeles Times*, Janda la Nyakati, Aprili 18, 1990.

ulaya katika mwaka wa 1850 aliongea kuhusu marekani kuwa kama serikali ya ajabu ambayo "imetoka" na "kati" ya kimya cha dunia ikiongeza nguvu zake na uwezo wake kila siku. *The Dublin Nation*.

Hizi "pembe mbili" kama mwanakondoo zinaakilisha tabia halisi ya taifa letu (marekani) jinsi inavyoonyesha katika misingi yake miwili-serikali na Dini misingi hii miwili ndio siri ya nguvu zetu na kukua kama taifa. Wale wa kwanza kupata maficho katika pwani za marekani, walifurahia ya kwamba walikuwa wamefikia taifa lilo huru kutokana na kiburi ambacho upapa ulikuwa ukidai na umabavu wa utawala wake wa kifalme. Walikusudia kuunda serikali ilio chini ya msingi pana wa serikali na uhuru wa dini.

## *Ananena Kama Joka*

LAKINI huyu mnyama aliye na pembe kama mwana kodoo " akaongea kama Joka" naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake, naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake, wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona. Akiwaambia wakao juu ya nchi, kumfanyia sanamu yule mnyama aliye na jeraha la upanga naye akaishi Ufunuo 13:11-14.

Yule mnyama mwenye pembe kama ya mwana kondoo na sauti ya joka ni mfano unaolenga tofauti halisi kati ya madai na matendo ya taifa linaloakilishwa. "kuongea" kwa taifa ni kitendo cha wanasheria na haki za utawala. Kwa tendo kama hilo litaonyesha uongo kwa misingi ya uhuru na amani ambavyo vimewekwa kama msingi wa utawala wake. Utabiri kuwa atanena, "kama joka na kutumia uwezo wa yule mnyama wa kwanza, hudhihirisha wazi kukua kwa roho wa mateso na asiyefumilia ambayo ilionyeshwa na mataifa yanayoakilishwa na joka na mnyama mfano wa chui. Na kwa habari ya kwamba yule mnyama mwenye pembe mbili " awafanya dunia na wakaao ndani yake kusujudu mnyama wa kwanza? Huonyesha kuwa uwezo wa taifa hili ni kulazimisha wengine kwa kuabudu ambalo ni tendo la kuutukuza upapa.

Tendo kama hili ni kinyume kabisa na misingi ya serikali hii kwa uelekevu wa vituo vyake huru na ni kinyume katika kuapa kwa kutangaza uhuru wake katika muungano.

Wanzilishi wa taifa hili walitafuta kwa hekima sana kulinda utumishi wa nguvu za kiserikali dhidi ya kanisa, na matokeo yake yasiyo epuka mateso na kutovumilia serikali husema ya kwamba, "Bunge kuu la marekani haitafanya sheria yo yote kwa kupendelea kuw-eko kwa dini ama kuweka vikwazo juu ya kulipa kodi," Na ya kwamba hakuna jaribu la kidini litakalohitajika kama kuhitimu katika ofisi yo yote ya raia walio chini ya muungano wa mataifa." Ila tu kwa uvunjaji wa sheria kwa taifa huru, Ndipo ibada ya dini yo yote yaweza kulazimishwa na mamlaka ya kiserikali. Lakini mageuzi ya matendo haya siyo makubwa tena kuliko inavyoonyeshwa kwa mif-ano. Ni yule aliye na pembe kama ya mwana kondoo anayedai kuwa msafi mtulivu na asiyedhuru. Ndiye anayenena kama joka.

## *Sanamu ya Mnyana*

AKIWAAMBIA wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama," Hapa imeonyeshwa wazi mfano wa serikali ambayo kwayo nguvu za kisheria zinadumishwa na watu, ni ushahindi wa ajabu ya kwamba marekani ni taifa linalotajwa katika unabii.

Lakini ni nini, "Sanamu ya mnyama" na itafanywaje? Sanamu




inayoitwa alama ya mnyama mwenye pembe mbili. Na pia ndio inayoitwa alama ya mnyama. Kwa hivyo kujifunza jinzi sanamu ilivyo na jinzi itakavyo fanyishwa ni laziwa tujifunze tabia zoteza mnyama mwenyewe yaani Upapa.

## *Muungano wa kanisa na serikali.*

WAKATI kaniza lile la kwanza lilichafuka kwa kujitenga kwa ukweli wa injili, na kukubali kanuni za kishenzi na desturi zao, likapoteza roho na nguvu za Mungu; na kwa kuyatawala mawazo ya watu, likatafuta msaada wa nguvu za kiserikali. Matokeo yake yalikuwa ni upapa, kanisa liliotawala nguvu za serikali na likaitumia kwa kutimiza malengo yake, hasa kwa kuadhibu "uzushi". Ili marekani ipate kufanyisha sanamu ya mnyama, uwezo wa kidini, ni mpaka pia itawale serikali ili mamlaka ya nchi yapate kutumiwa na kanisa kwa kutekeleza malengo yake.

Ilikuwa ni uasi ulioliongoza lile kanisa la kwanza kutafuta msaada wa serikali, na hili jambo likaandaa njia kwa kukuwa kwa upapa - yule mnyama. Kwa hivyo uasi ndani ya kanisa utaandaa njia ya sanamu ya mnyama.

## *Historia Kujirudia Tena*

BIBILIA inasema kwamba kabla ya kuja kwa Bwana, kutakuwa na hali ya kupotoka kwa dini sawa tu ile uliotokea katika karne za kwanza. "Siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukurani, wasio safi, wasio wapenda wakwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasio penda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake." 2 Timotheo 3:1-5. "Basi roho anena waziwazi ya kwamba, nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Wakati hali hii ya uovu itakapofikia, matokeo sawa yatafuata kama yale ya karne za kwanza.

## *Kufanyishwa kwa sanamu.*

WAKATI makanisa makubwa ya marekani, yatakapo ungana pamoja kwa mambo ya mafudisho jinsi wanavyoyashikilia wao pamoja, wataisukumia nchi kulazimisha maamuzi yao na kusimamisha desturi zao, ndiposa Amerika ya kiprotestanti itakuwa imefanyisha sanamu ya utawala wa kirumi, na mateso ya serikali kwa wale wote wasiokubaliana bila shaka itakuwa ni matokeo yake.❑

# ALAMA YA MYAMA

MNYAMA aliye na pembe mbili "Awafanya" [Kuamrisha] wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume au katika vipaji vya nyuzo zao. Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani jina la mnyama yule au hesabu ya jina lake" ufunuo 13:16-17. Onyo la malaika watatu ni mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa kwa mvinyo ya ghadhabu ya Mungu" mnyama ambaye ametajwa katika habari hii, ambaye ibada yake italazimishwa na mnyama mwenye pembe mbili, ni wa kwanza au aliye na mfano wa chui mnyama wa ufunuo 13- upapa. "Alama ya mnyama" huakilisha tu hali ya uprotestanti ambao umeasi ambao utakuwa wakati makanisa ya kiprotestanti yata-tafuta msaada wa nguvu za kiserikali kwa kulazimishia watu mafundisho yao. Alama ya mnyama" bado haijatafsiriwa.

## Tofauti ya ibada

BAADA YA onyo juu ya kumwabudu mnyama na sanamu yake unabii unasema. "Hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya yesu, Ufunuo 14: 12. kwa vile wale wanaozishika amri za Mungu hao hubainishwa pamoja na wale wanao mwabudu mnyama na sanamu yake na kupokea alama yake basi inafuata ya kwamba, kwa kushika sheria za Mungu upande mwingine na kuzivunja kwa upande mwingine, kutofautisha kati ya wanaom-wabudu Mungu na wale wamsujuduo mnyama.

## Tabia ya mnyama

TABIA ZA kipekee za yule mnyama basi na alama yake, ni kuvunja amri za Mungu. Danieli asema kwa yule pembe ndogo. "Upapa:" Ataazimu kubadili wakati na sheria,"Danieli 7: 25 Na paulo naye ametafsiri nguvu hizo kama "mtu wa kuasi" ambaye angejiinua juu ya Mungu. Unabii moja ni mwisho wa unabii mwingine. Ni kwa kuibadili sheria ya Mungu upapa ukapata kujiinua juu ya Mungu.Yeyote awezaye kwa kuelewa kutunza sheria jinzi imebadilishwa ni kumpa heshima kuu uwezo huo ulioibadilisha. Kitendo kama hicho cha kutii sheria za kipapa ni kama alama ya mapatano kwa papa katika pahali pa Mungu.

Kusudi la shauriano katika badiliko limeonyeshwa: "ataazimu kubadili majira na sheria" badiliko katika sheria ya nne hutimiza unabii kamili. Kwa badiliko hili ni mamlaka inayodaiwa na kanisa. Hapa uwezo wa kipapa unajionyesha wazi juu ya Mungu.

## Utakatifu Wa Jumamosi

HUKU wanaomwabudu Mungu watakapokuwa wamebainishwa kwa kuitunza sheria ya nne kwa vile hii ni ishara ya uwezo wa uumbaji na ni ushahidi wa Mungu kwa madai yake juu ya heshima na sujudu za mwanadamu wanao-mwabudu yule mnyama wataba-inishwa kwa juhudi zao za kuhar-ibu ukumbusho wa muumba, kwa kuiinua sheria za Rumi. Ilikuwa ni kwa ajili ya jumapili ya upapa ukaingiza madai yake ya kikaidi, na juhudi zake za kwanza za kutafuta uwezo wa serikali, ilikuwa ni kulazimisha pumziko katika siku ya jumapili kama, "siku ya bwana". Lakini Bibilia huonyesha wazi hulenga siku ya saba, na siyo siku ya kwanza, kama siku ya bwana"Basi mwana wa adamu ndiye Bwana wa sabato pia". Sheria ya nne inatangaza "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana" Na kupitia kwa nabii isaya Bwana anatangaza "Siku ya Utakatifu wangu". Mariko 2:28; Isaya 58:13.

Wakatoliki wa kirumi wana-kubali ya kwamba badiliko la Sabato lilifanywa na kanisa lao, na wanatangaza ya kwamba waprotestanti kwa kuitunza Jumapili wanakubaliana na uwezo wake.

Kama ishara ya mamlaka ya kanisa katoliki, wandishi wa kanisa la kirumi wanena "kitendo hicho cha kuibadilisha Sabato kwenda jumapili, ambacho waprotestanti wanakubaliana nacho kwa Sababu kwa kuitunza jumapili, wanakubali uweza wa kanisa kwa kuchagua sherehe na kuwaamrisha hao chini ya dhambi." - Henry Tuberville, an abridgment of the christian doctrine, pg 58. Basi nini badiliko la sabato, lakini ishara, au alama, ya mamlaka ya kaniza la kirumi - "Alama ya mayama" ?



## Kukataa Biblia

KANISA la kirumi halijaachilia madai yake ya utawala; na wakati ulimwengu na makanisa ya kiprotestanti yatakubali sabato yake, huku wakiikataa Sabato ya bibilia, wanakubaliana na madai haya. Wanaweza kudai mamlaka ya kidesturi na ya mababa zao kwa kubadilisha; lakini kwa kufanya hivyo wanapuuza maagizo ambayo yanawatenga kutoka Rumi ya kwamba "bibilia ni bibilia pekee ndio dini ya waprotestanti." Waf-uasi wa kanisa la kirumi waweza kuona ya kwamba wanajidanganya wenyewe, wakijipenda wenyewe kuyafunika macho yao katika ukweli katika jambo hili. Jinzi mwendo wa kulazimisha jumapili utakapopata pendekezo, wafuasi wa kanisa la kirumi watafurahia, wakijisikia kuhakikishiwa kuwa mwishowe Rumi italeta ulimwengu wa waprotestanti kuwa chini ya Bandera ya Rumi.

## Kusujudu Mnyama

LAKINI wakristo wa vizazi vimeshapita walitunza jumapili, wakidhania ya kwamba kwa kufanya hivyo wanatunza Sabato ya Bibilia; na sasa hivi kuna wakristo wa kweli katika kila kanisa, bila kuacha mbali ushirika wa katoliki ya kirumi, wale ambao huamini kabisa ya kwamba jumapili ni sabato iliotengwa kando na Mungu. Mungu hukubali unyofu wao na msimamo wao mbele yake. Lakini wakati Jumapili itakapopitishwa kisheria na ulimwengu kuangaziwa kuhusu umuhimu wa Sabato ya kweli, basi ye yote atakayevunja sheria za Mungu kwa kukubali maagizo ambayo hayana uwezo wowote isipokuwa tu huo wa Rumi basi yeye atakuwa anauheshimu upapa kuliko Mungu. Anatoa heshima kwa Rumi na kwa uwezo ambao unaolazimisha sheria za Rumi. Yeye anaabudu yule mnyama na sanamu yake. Jinsi watu watakavyokataa maagizo ya Bwana ambayo ametangaza kuwa ni ishara ya mamlaka yake, na badala yake kuiheshimu ile ambayo Rumi imechagua kama msemo wa utawala

**"Sisi, kama serikali ya kanisa katoliki ya kirumi, tunataraji watoto wote walio waaminifu kwa kanisa kumsaidia Raisi kwa nguvu zetu zote kuona ya kwamba watu binafsi washirika wa mahakama kuu ya marekani wametii masharti ya Raisi. Na, ikiwezekana, tutabdilisha, rekebisha na hata kuondoa katiba ya sasa, ili Raisi aweza kupitisha yaliyo yake au mipango yetu ya kiutu na haki zote za kibinadamu jinzi zimetolewa na mtakatifu papa na kanisa takatifu.**

**"Tulimchagua Raisi wetu anayefaa. Tutatengeneza sheria zetu na kuzipitisha kulingana na uongozi wa yule mtakatifu, na papa na sheria ya mamlaka ya papa. Mjengo huu wote ni mpaka ujengwe upya katika msingi huu. Kanuni zetu za kielimu ni lazima zitafsiriwe mpaka mwisho ili ukafiri, hatari ya mafundisho mabaya, uprotestanti, ukomunisti, ujamaa na mengine yote kama hayo yataka-nyagwa na kurushwa mbali na inchi."** *La Aura Magazine*, Italian Baptist Publishing Association, Philadelphia, PA.

**Marekani Yabadilisha Katiba — Yaidhinisha Sabato ya Upapa — Yaongea Kama Joka.**




wake, Basi watakuwa wamekubali ishara ya mapatano kwa Rumi - " Alama ya mnyama".Na sio mpaka tu wakati jambo hili litakapowekwa wazi mbele ya watu, na kuletwa kuchagua juu ya sheria za mungu na maagizo ya wanadamu, ili ya kwamba wale wanaoendelea kwa uasi wanaoendelea kwa uasi watapokea "alama ya mnyama."

### *Tisho la Kuogofisha*

TISHO LILE la kuogofya sana ambalo halijawahi kutan-gazwa kwa binadamu ni ile lipatikanalo katika ujumbe wa malaika wa tatu. Hiyo itakuwa ni dhambi ya kutisha inayoleta ghadhabu ya Mungu isioch-anganywa na rehema yake. Watu hawajaachwa gizani kuhusiana na jambo hili, onyo juu ya dhambi hii itatolewa kwa ulimwengu wote kabla ya hukumu za mungu kuanguka, ili wote wajue ni kwa nini watateswa, na wana nafasi ya kuepukana nayo. Imedhi hirishwa wazi katika unabii kwa kutangazwa kwa sauti kuu, na

> **"Utunzaji wa jumapili kwa waprotestanti ni heshima wanaotoa kwa kupenda kwao wen-yewe, kwa mamlaka ya (kanisa) katoliki."** Mosignor Segur, *Plain Talk About the Protestantism of Today*, page 213.

malaika anayepita katikati ya mbingu; na onyo hili litaamsha mawazo ya ulimwengu.

### *Kukua Makundi Mawili*

KATIKA matokeo ya vita ukristo wote utagawanyika katika makundi mawili-wale watunzao sheria za Mungu na imani ya Yesu na wale wamsujudio mnyama na sanamu yake na kupokea chapa yake. Hata ingawa kanisa na serikali wataunganisha nguvu zao ili washurutishe "wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini na walio huru kwa watumwa" (ufunuo 13:16), wapokee chapa katika vipaji vya nyuzo zao hata hivyo watu wa Mungu hawataipokea. Nabii wa patimo aliwaona "wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama na sanamu yake na kwa hesabu ya jina lake walikuwa wamesimama kando kando ya hiyo bahari ya kioo wenye vinubi vya, Mungu". Nao wauimba wimbo wa musa mtumwa wa Mungu na wimbo wa mwana kondoo. Ufunuo 15 : 2-3.

### *Madanganyifu Mawili Makubwa*

KUTOKANA na madhanganyifu mawili makubwa, kutokufa kwa mtu wa asili na kutakaswa kwa Jumapili, shetani atawalete watu chini ya udaganyifu wake. Huku la kwanza likiwa linaweka msingi wa imani kwa roho za mizimu, la pili litalete muungano pamoja na Rumi. Waprotestanti wa nchi za marekani watakuwa wa kwanza kunyoosha mikono yao kwa lile pengo kubwa ili kushika mkono wa roho za mizimu, watan-yoosha mkono wao juu ya shimo kubwa ili kushikamana na uwezo wa kirumi; na chini ya muungano wa hawa watatu, nchi hii itafuata nyayo za Rumi kwa kukanyagia chini uhuru wa dhamira.

Mpaka wa kubainisha kati ya wanaokiri kuwa ni wakristo na waovu ni vigumu sana kutofautisha. Washiriki wa kanisa wan-apenda yale dunia inapenda na wako tayari kuungana pamoja nao, na shetani amekusudia kuwa-unganisha wote katika muungano moja, na kwa hivyo apata kujipatia nguvu akiwafagilia wote katika daraja za kuamini mizimu. Waf-uasi, wa Rumi wajisifuo kwa miujiza, kuwa ishara kamili ya kanisa la kweli hao watakuwa tayari kudanganywa na nguvu hizi za kufanya miujiza, na waprotestanti wakiwa wameachilia mbali ngao ya kweli, hao pia watadanganywa. Wafuasi wa Rumi, waprotestanti na watu wa ulim-wengu wote watakubali tu mfano wa utauwa usio na nguvu, na wataona katika huu muungano mwendeleo mku-bwa wa kuiongoa dunia na kuwafungulia siku elfu moja za raha zilizo tarajiwa kwa muda mwingi.❏

# Shetani Kulazimisha Mpango wa Ulimwengu Mpya

KUPITIA KWA roho za mizimu, shetani ataonekana kuwa kama mfadhili wa kizazi, akiponya magonjwa ya watu na kujifanya kana kwamba analete hali mpya na ya juu ya imani ya kidini, lakini kwa wakati huo akifanya kazi kama mwangamizi. Majaribu yake yawaongoza wengi kwa udanganyifu. Kutokuwa na kiasi hupumbaza akili, tamaa ya mwili, vita na umwagikaji wa damu ni matokeo yake. Shetani hufurahia vita kwa vile vinaamsha tamaa mbaya ya moyo na kuwafagilia milele wale wote ambao ni mateka wake waliojiingiza katika uasherati na umwagikaji wa damu. Ni kusudi lake kuamusha mataifa ili kupigana wao kwa wao, kwa vile kwa njia hiyo aweza kupotosha mawazo ya watu kwa kazi ya maandalizi katika siku ya Bwana. Shetani hufanya kazi kupitia kwa vitu vya kuonekana kwa roho ambazo hawako tayari. Amejifundisha siri ya uvumbuzi wa maumbile na hutumia nguvu zake zote kwa kutumia maumbile hata kiwango kile Mungu anapomkuba-lia. Aliporuhusiwa kumtesa ayubu, ni kwa haraka gani mifugo na malisho, wajakazi, majumba, watoto, walifagiliwa mbali, shida moja ilifuata ingine kama kwa dakika. Ni Mungu anayewakinga viumbe vya-ke na kuwazingira kutokana na nguvu za mwangamizi. Lakini ulimwengu wa wakristo wameonyesha madharau kwa sheria za Yehova na mungu atatenda ile ambalo amelitangaza kuwa atalitenda ataondoa mibaraka yake katika ulimwengu na kuondoa kinga yake ya ulinzi kutoka kwa wale wanaoenda kinyume cha sheria yake, na kufundisha wengine kufanya sawa na hawa. Shetani anatawala wale wote ambao hawako chini ya ulinzi wa Mungu. Atapendekeza na kuwafanikisha wengine ili kutimiza matakwa yake, na atawaletea wengine taabu na kuwaongoza waamini ya kwamba ni Mungu anayewatesa. Huku akionekana kati ya watu kama tabibu mkuu awezaye kuponya magonjwa yao yote, ataleta mag-onjwa na uharibifu mpaka miji mik-uu isoroteke kwa kuangamizwa na kuharibiwa.

> **"Ilichukuwa upapa na mashirika yake yote, kanisa katoliki la kirumi, karibu miaka yote ya 2000 kuufikia utimilivu na hali yake ya kisiasa.... Na lengo la kisiasa na ujenzi? ndiyo, na lengo la kisiasa na ujenzi. Kwa maana utafiti wa mwisho, yohana Paulo wa II kama vile anavyodai kuwa mwakilishi wa kristo amedai kuwa yeye ni hakimu mkuu katika jamii ya kimataifa."** *Keys of This Blood*, M. Martin, pages 374- 375.




### *Waasi Kutambulika*

NA BASI ndiposa yule mdanganyifu mkuu atawashawishi watu ya kwamba wamtumikiao Mungu ndio waletao shida hii. Lile kundi ambalo limeikasirisha mbingu watatoa lawama kwa wale wote ambao utiifu

wao kwa sheria za Mungu ni kemeo ya milele kwa waasi. Itatangazwa ya kwamba watu wanaomkosea Mungu kwa kuvunja Sabato ya jumapili, ya kwamba hii ndio dhambi inayolete maafa ambayo hayatakoma mpaka kutakaswa kwa jumapili kutakap-otiliwa mkazo, na ya kwamba wale wanafundisha madai ya kutunza amri ya nne, basi kuvunja utakatifu wa jumapili, hao ndio wataabishi wa watu, wakizuia kurejeshwa kwa wema wa Mungu, na kuendelea kwa muda. Nguvu za kazi ya miujiza ikifunuliwa kupitia kwa roho za mizimu italete mvuto wake juu ya wale wamechagua kumheshimu Mungu kuliko wanadamu. Mawa-siliano kutoka kwa roho wachafu watatangaza ya kwamba Mungu amewatuma kuwahakikishia wale ambao wanakataa kutunza juma-pili kwamba wamekosea, na kuw-adhibitishia ya kwamba sheria za nchi ni sharti zitunzwe sawa na sheria za Mungu. Watalilia uasi mkuu duniani na kurudia ushuhuda wa waalimu wa dini ya kwamba kupungua kwa hali ya tabia kumesababishwa na kutotunza jumapili. Hasira kali itaamshwa juu ya wale wote wanaokataa kukubali ushuhuda wao. ❏



## Ujumbe wa Malaika wa Tatu

**"Na mwingine, malaika wa tatu, akafutata, akisema kwa sauti kuu, mtu awaye yote akamsujudu huyo myama na sanamu yake na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake au katika mkono wake yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyolengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika na mwana kondoo: Na moshi wao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana au usiku, hao wamsujuduo huyo myama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake."** Ufunuo 14: 9-11 (kwa maelezo kamili usome vita kuu).

# SHETANI KUJIFANANISHA KRISTO

KAMA TENDO la hali ya juu katika mchezo wa udanganyifu shetani mwen-yewe atajifananisha kristo. Kwa muda mrefu kanisa limekuwa likidai kungojea kurudi kwa kristo kama mwisho wa tumaini lake. Sasa mdanganyifu mkuu ataifanya kuonekane ya kwamba kristo amekuja. Katika sehemu mbali mbali za dunia, shetani atajionyesha katikati ya watu kama kiumbe chenye nguvu ya kustaajabisha, akijifananisha na hali ile ile ya mwana wa Mungu jinsi yohana ametaja katika ufunuo Rev 1:13-18. Utukufu unaomzunguka ni ule usiozidi cho chote ambacho macho ya mwanadamu amewahi kuona. Sauti ya shangwe ikasikika juu angani "kristo amekuja! kristo amekuja!" watu wataanguka chini katika heshima mbele yake, huku akiinua mikono na kutangaza mibaraka juu yao, jinzi kristo aliwabariki wanafunzi wake wakati alipokuwa hapa duniani. Sauti yake ni nyororo na laini huku imejawa na nyimbo za furaha. Katika utulivu, sauti za huruma atatoa baadhi ya kweli zingine za mbinguni ambazo mwokozi alitoa; ataponya magonjwa ya watu, na katika tabia yake ya kujifananisha na kristo atadai ya kuwa ndiye aliyeibadilisha sabato kwenda jumapili na ataamrisha wote waabudu siku ile ameibariki.

Atatangaza ya kwamba wale wanaosizitiza kutunza takatifu siku ya saba ya sabato hao wanalikufuru jina lake kwa kukataa kusikiza malaika waliotumwa kwao na nuru na ukweli. Huu ndio udanganyifu mkubwa wa hali ya juu. Kama vile wasamaria walivyodanganywa na simoni, umati mkubwa tangu mdogo hata mkubwa wakamsikiliza huyu mchawi, waki-sema:"Huu ni uwezo wa Mungu, ule mkuu". Malendo 8:10.

> **"Ilichukuwa upapa na mashirika yake yote, kanisa katoliki la kirumi, karibu miaka yote ya 2000 kuufikia utimilivu na hali yake ya kisiasa.... Na lengo la kisiasa na ujenzi? ndiyo, na lengo la kisiasa na ujenzi. Kwa maana utafiti wa mwisho, yohana Paulo wa II kama vile anavyodai kuwa mwakilishi wa kristo amedai kuwa yeye ni hakimu mkuu katika jamii ya kimataifa."** *Keys of This Blood*, M. Martin, pages 374- 375.

### *Kuitambua Huyu Mdanganyifu*

LAKINI WATU wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya huyu kristo wa uongo hayamo sambamba na maandiko. Mibaraka yake, itatangazwa juu ya wasujuduo mnyama na sanamu yake. Kundi hilo hilo ambalo Bibilia inasema ya kwamba juu yao ghadhabu ya Mungu isiochanganywa na maji itawaangukia. Na zaidi, ya hayo, shetani hajaruhusiwa kuiga namna ya kurudi kwa kristo. Mwokozi amewaonya watu wake kuhusu uongo juu ya jambo hili, na ametangulia kusema dhahiri jinsi ya kurudi kwake mara ya pili. "Kwa maana watatokea wakristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini hata walio wateule..... Basi akiwaambia, yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani msisadiki, Kwa maana kama vile umeme utokavyo mash-ariki ukaonekana hata magh-aribi hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwa mwana wa adamu". Mathayo 24 : 24 - 27, 31 ; 25:31. Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4: 16-17. Kuja kwa hali kama hii hakuna uwezekano wa kuuiga. Kutaju-likana na watu wote - ukishuhudiwa na ulimwengu wote.

### *Ni Bibilia Tu*

WALE TU ambao wamekuwa wasomi wa maandiko na wale wamepokea kuipenda kweli watazingirwa kutokana na udanganyifu mkubwa utakaochukuwa ulimwengu mateka. Kwa ushuhuda wa Bibilia hawa watamtambua mdanganyifu na hila zake. Kwa wote saa ya kujaribiwa itawajilia. kwa kupepetwa na majaribu wakristo wa

**"Lengo la mwisho la ulimwengu wote kuja pamoja, jinzi wakatholiki wanafikilia, ni umoja wa imani, ibada, na kutambua mamlaka kuu ya kiroho ya askofu wa Rumi."** Prist J. Cornell.





kweli watafunuliwa. Je watu wa Mungu sasa hivi wamejipanga imara katika neno lake ili wasije wakajitoe kwa ushahidi wa mawazo yao? Yawezekana, katika pambano kama hilo waishikilie biblia na bibilia pekee? Itawezekana apange mambo ili awazuie kutopata maandalizi ili kusimama katika siku hiyo. Atapanga hali ya mambo, ili kuwafungia njia, kuwanasa na mali ya dunia kuwafanya wabebe mizigo mikubwa ya kuchosha, na siku hiyo iwajilie juu yao kama mwivi.❏

## MADAI YA RUMI

**"MWANDISHI** wa *The Catholic Mirror* ya Baltimore, MD, alichapisha mfululizo wa habari za waandishi wengine wanne, Zilizoonekana katika jarida la Septemba 2, 9, 16, na 23, 1893. Basi, nakala hizi hata ingawa hazikuandikwa na mkono wa askofu (Gibbons) mwenyewe, bado Zaonekana kuidhinishwa chini ya amri yake, na zina usemi wa kipapa katika jambo hili, haya ni madai yalio wazi ya upapa kwa uprotestanti, na ni madai ya upapa ya kwamba waprotestanti watatoa kwa upapa Sababu ya hao kuitunza Jumapili....

"Waadventista ndio tu jamii ya wakristo walio na Biblia kama mwalimu wao, ambao hawawezi kupata thibitisho katika nakala zake kwa kuibadilisha siku kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza. Kwa hivyo, Jina lao ni Waadventisha wasabato.' Waprotestanti....wameikataa siku iliotajwa na Mungu kwa ibada yake, na wakakubali dhahiri kupigana na Amri yake Mungu, siku ya ibada yake ambayo haijawahi kuruhusiwa kwa kusudi hilo, katika nakala za Bibilia....

"Lakini kwa kweli, bila shaka, na kwa uadilifu busara halisi ya haki hukana lawama kwa kundi hili ndogo (Waadventista wa sabato ambao hesabu yao leo ni zaida ya millioni 8) bila uchunguzi kamili....

"Ulimwengu wa uprotestanti umekuwa kutoka utotoni mwake, katika karne ya 16, ukishikamana kabisa na kanisa la katoliki, katika kuitakasa Jumapili wala si Jumamosi.

"Ikiwa...kwa upande mwingine, (Waisraeli na waadventista) wa kisasa watatoa malalamishi yalio kinyume cha Jamii kubwa ya Waprotestanti...(Waprotestanti)...hawana njia ingine tena ilisalia ila tu ni kukubalia kwamba wamekuwa kwa muda wa karne tatu wakifundisha na kutenda yalio kinyume cha maadiko....Kwa kuongezea katika zito wa andiko hili na kosa lisilo sameheka, umesababisha kuwekwa mkazo katika moja yapo ya amri za Mungu kwa mtumishi, wake mwanadamu: "Ikumbuke siku ya sabato uitakase." (siku ya saba) Hakuna waprotestanti, (ila tu waadventista wengine wachache) wanaoishi hivi leo ambao wameshakubali kuitii sheria hiyo, wakipendelea kufuata kanisa ambalo limeasi kuliko kumfuata mwalimu wao yaani Bibilia, ambayo kutoka mwanzo hadi ufunuo haifundishi mafundisho mengine....." *Rome's Challenge*, 1-5.

"Huku mwisho hautaepukika, yaani, kwa wale wanaoifuata Bibilia kama kiongozi wao, waisraeli na waadventista wanao ushahidi wa kutosha kwa upande wao, huku waprotestanti wa Bibilia hawana neno hata moja la kujikinga katika kuibadilisha Jumapili kutoka Jumamosi." *Romes Challenge*, 11. ❏

# Ni Nini Cha Kufanya Sasa

**K**ATIKA kiwango hiki na tugeuze macho yetu kutoka kwa historia ya yaliopita na pambano lililo mbele yetu, na tutazame kiini cha mambo sasa . Waweza kuwa mtoto wa Mungu sasa hivi - dakika hii - ikiwa utataka. Mungu ameyafanya yote ambayo yamempasa kufanya, mpaka tu ukubali yale ambayo ameyatenda. Mungu anakupenda sasa "hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele " yohana 3:16.

### *Nguvu ya Kuwezesha*

**J**E UMESHAPOKEA kipawa hicho? wote wampokeao hupewa nguvu ya kufanyika watoto wa Mungu "Bali wote walio mpokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake," yohana 1:12 wewe ni wa Mungu. Alikuokoa Kwa hivyo wewe ni wake katika wokovu lakini hatakulazimisha; ni lazima uchague kuwa wake; ni lazima ukubali haki yake, na uhusiano wako, ujitoapo kwake, basi wewe ni wake. Tazama warumi 6 :16. Dakika ile ile unapotoa maisha yako kwa uongozi wake,dakika hiyo hiyo yeye hukuongoza. Basi huwa dakika - kwa dakika kutembea na Mungu. Ukiongozwa naye, wewe ni mtoto wake. " Kwa kuwa wote wanaongozwa na roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu." Warumi 8 : 14.

Je, unajua ya kwamba dhambi ni uvunjaji wa sheria za Mungu? "Kila atendaye dhambi, afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi" 1 Yohana 3:4, Tazama pia warumi 5 :13 na 7:7.

Je, unajua ya kuwa siku ya saba ni sabato ya Bwana? "Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibariki siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kufanya," Mwanzo 2:2-3. Tazama pia kutoka 20 : 8-11.

### *Kuzaliwa Upya*

**K**WA RAFIKI wa dunia tunafanya uhusiano kwa kuonana ama kusalimiana. Kwa Yesu tunaungana kwa mawazo yetu. Amini neno la Mungu. Amini katika roho yako. Tanzama warumi 10:10 Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la kristo "Warumi 10 : 17. Ndipose imami ya Yesu huja kwa

kujifunza neno la Mungu. Tazama ufunuo 14:12. Ni lazima tujitahidi kijionyesha kuwa tumekubalika na Mungu, na ndipo tutii ukweli wa nyakati hizi. Tazama 2 Timotheo 2: 15. Ndipo neno (ndani ya moyo wako ) huanza maisha mapya, ambayo ni " kuzaliwa upya" Tazama 1 Petro 1:23. Ndipo, uendelee kunywa maziwa ya neno na kwa hivyo "Kukua". Tazama 1Petro 2:2. Usisubiri kujisikia fulaha. Mungu katika neno lake, haijalishi unajisika vipi.❏

### *Kutakaswa ni Sasa*

KWA KUPENDA kutii katika amri za Mungu upendo wetu kwake unaonekana. "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua wala hazishiki amri zake, ni muongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake " I yohana 2:3-5. Cho chote utakacho, mwomba Mungu, na umshukuru Mungu kwa hicho. Sasa ni chako. Tazama mariko 11:24. Hata ingawa ni lazima upewe kulingana na mapenzi ya Mungu. Tazama I yohana 5:14-15.

Mungu asema, "Nitawatakazeni na uchafu wenu wote." "nami nitawapa ninyi moyo mpya". " nami nitatia roho yangu ndani yenu" Ezekieli 36:25-27. Muulize Mungu akufanyie hivyo. Mshukuru yeye ya kwamba imefanyika hivyo, kwa sababu ameahidi. Kiri dhambi zako kwake. Muulize akusamehe umushukuru kwa vile amelifanya. I Yohana 1:9, Mathayo 7:7, 11, wafilipi 4:6, 19. Bibilia imejawa na ahadi; zote ni zako, kuhusu mpango huu rahisi.

### *Tembea na Kristo*

JE MSOMAJI mpendwa Mungu anakutaka uwe mtoto wake? Jibu ni ndio, ndio! ndio! sasa swali ni hili, Je, msomaji mpendwa, ungependa kuwa mtoto wa Mungu? Ikiwa jibu lako ni ndio, basi katika nguvu za neno la Mungu, wewe ni mtoto wa Mungu. Weka mkono wako kwake na ukae naye. "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini mtumaini Bwana siku zote, Maana Bwana Yehova ni mwamba wa milele. Isaya 26:3-4. ❏

## Msomaji, wewe utafanya nini?



## The Great Controversy

Agiza hivi leo kitabu kizima chenye kurasa arobaini na mbili ambacho kutoka ndani yake, mengi ya jarida hili la sasa yameelez wa chunguza kwa kindani mambo yanayohusiana na matukio ya nyakati nyingi nyuma ya pasia ya pambano kati ya nguvu za mema na mabaya. Kitabu hiki kinasististhia sana matukio muhimu katika zana zote za kikristo kuelekea kwa utisho unaokuja haraka kufikia kilele chake. Kimejawa na historia na maandiko ya Bibilia. Vimeuzwa kwa mamilioni uliwenguni kote. Vingi vikiwa na rangi nne tofauti juu ya jalada zake. Kikiwa kimelipiwa gharama ya pasto katika marekani na nchi zilizo chini ya hima yake. (English only).




**US $4.95**
**postage paid**

## Mafundisho ya bure ya Biblia

Ikiwa unatafuta majibu kwa maswali haya yote ambayo ni ya muhimu na ya kutisha, utume kadi yako ya kuitisha mafundisho ya bure ya bibilia. Hakuna malipo kwako na hakuna uzito wa maarifa Badala yake utapata kweli zilizo rahisi kuelewa za Bibilia ambazo zitakusaidia kuja kuelewa maana zaidi ya Bibilia.

## Muhtasari wa Mchapishaji

Jarida hili limechapishwa kwa msaada wa matoleo na sadaka. Ikiwa utapenda kusaidia mradi huu, tuma hundi au hawala ya pesa zote zilipwe kwa Heralds of truth. Tafadhali onyesha ya kwamba pesa zako ni za kusaidia Jarida la onyo la mwisho wa dunia."

"Maoni kuhusu yaliomo ndani ya Jarida hili yaweza kutumwa kwa anwani ambayo imetolewa hapa chini yakielekezwa kwa. Mwandishi.

# Onyo la Mwisho kwa Ulimwengu

AMANI DUNIANI" ni jambo lijulikanalo sana mara moja kila mwaka na ulimwengu wa wakristo washerekeapo krismasi. Kwa kweli kila mahali watu wazuri hakuna wanachotamani sana kama vile kuwa na amani duniani ili wapate kuonja furaha ya jamii, imani, marafiki na mshahara wa kazi yao nzito. Lakini ni vipi amani ya dunia inaonekana ya kudanganya!

Kwa miaka ya nyuma dunia imekuwa na nyakati za vipindi mbali mbali ya kupumzika kisiasa na kijamii katika wakati wa milki za dunia kama vile babeli, wamedi na wajemi, wayunani, na warumi katika historia ya kwamba wakati wa kuanguka kwa milki ya Rumi, ulaya iligawanyika mataifa kumi mbali mbali. Zaidi karne nyingi maelfu na hata mamilioni ya watu wame-angamia, kwa vile mashujaa mbali mbali wenye nguvu wamejitahidi bila kufanikiwa katika kukusanya pamoja tena nchi hizi kumi.

Vita vya kwanza vya dunia vilipiganwa "kumaliza vita" ubatili wa madai hayo uliwekwa wazi na mteketeo mkubwa wa vita vya pili vya dumia. Kwa kweli vita hii vya ulimwengu wote vilifikia mwisho tu, wakati ule fumbuzi na utumizi wa silaha za atomiki binadamu ame fumbua silaha zenye nguvu za kuangamiza na za kuogofya hivi kwamba tumehofia ya kwamba vita vyo vyote vyaweza kumalizia kwa maangamizi ya kinukilia vikiwa na uwezekano mkubwa wa kuang-amiza maisha ya watu katika sayari hii.

Amani kama matokeo ya hofu ya maangamizi imeonyesha pia kuwa haina nguvu. Hata katika tisho la uharibifu wa silaha za sumu dunia imeshuhudia wingi wa mapambano na silaha ndogo ndogo na mapambano mengine makubwa kama yale ya Korea, Vietnamu, na Afgha-nistani, Nguvu hizi mbili-urusi na marekani wamejiondoa katika hali ya kufunjika moyo kwa vita ambavyo hawange vishinda kwa silaha za kawaida




**Kuyeyuka kwa ukuta wa Berlin - 1989**

## Ni Nguvu ngapi Zimebaki?

pekee lakini waliogopa kuachilia silaha za sumu.

Katika hali hii ya kupambana kwa kulete umoja, na tumaini katika dunia hii, imechukuwa hatua na nguvu nyingi za kibinafsi kwa kutoa suluhisho ya mahitaji ya mwana-damu kwa amani na maendeleo. Katika oktoba 1978 Askofu asiy-eoo-nekana ambaye ni karoi wojtyla, alichaguliwa kuwa kiongozi wa kanisa katoliki na kiongozi wa mji mkuu wa vatikani. Papa wa wakati huu amejaribu sana kutumia mamlaka yake ya pili katika juhudi za kuingiza imani yake kuwa yeye in papa atakayerejea katika kiti cha utawala ulimwenguni, kiti ambacho mapapa walilazimishwa kuhama mnamo mwaka wa 1798 Katika mwisho wa zile zama za giza. Wengi wanamchukulia kuwa ni papa wa kwanza wa nyakati hizi aliye na uwezekano wa kutimiza lengo hilo. Kitabu kiitwacho (The keys of this blood) kilitangaza mlolongo wa matukio yanayo kusudiwa kuibadilisha dunia milele. Kinaonyesha washirika halisi katika matukio haya na mwisho wa kusudi lao. Kitabu hicho kinaendelea kusema "Papa Yohana Paulo wa II wanapigana na urusi na nchi za magharibi kwa lengo la kuongoza mpango wa ulimwengu mpya.

Mwandishi Malachi Martini mm-oja wapo wa mwanachana wa jamii ya dini yakirumi na mchunguzi wa mambo ya ndani ya vatikani, alipata kuona vile upapa unapambana kutawala ulimwengu. Kitabu hicho kinalete baadhi ya unabii unaohusu dunia katika siku za usoni, na kinaeleza sana maarifa ya vatikani kwa kuitawala dunia. moja yapo ya huo unabii unaonyesha maarifa ya papa katika kuiangusha nchi ya urusi. (USSR)

Kutimia kwa unabii huo sasa umeandikwa vizuri sana katika Historia. Chapa nyingi za dunia zimeitambua vizuri sana kazi na Jukumu la papa katika kuivunja kwa ukomunisti wa urusi jinzi imeonyeshwa katika kuanguka kwa Berlin wall Novemba 9, 1989.

Sasa muungano wa sovieti ya zamani ni mojayapo ya historia, washirika waliosalia katika pambano la kuvuta na hata kutawala watu wa kizasi cha mbele ni marekani, umoja wa mataifa na papa yohana wa 2. Bado inatazamiwa kuonekana ikiwa uchina ya kikomunisti itaendelea ama itaonyesha orodha ya kisiasa.

Kwa sababu ya mwandishi mmoja wa jamii ya dini ya kirumi anatabiri ya kuwa mpango wa ulimwengu mpya umekaribia, hiyo sio sababu ya kutosha ya kulete hofu isiofaa. Jambo la kuhofisha ambalo limetolewa katika kitabu cha Keys of this blood ni lile ya kwamba, liko sambamba na unabii ulioandikwa katika Bibilia muda wa miaka 2000 iliyopita.

Mpaka viwango vipi ambapo papa, umarekani na /au umoja wa mataifa watasikia msukumo wa kuenda kulete utulivu kwa mapambano yaonekanayo kuwa hayana mwisho katika dunia yetu ya leo? Ni sehemu zipi zitakazo chukuliwa kwa kulete amani kati ya ulimwengu wa sasa wa kijamii, kisiasa na msuko - suko wa kidini? Je, mpango wa ulimwengu mpya au serikali itasimama katika siku zetu za jitihada za kurudisha uhusiano wa dunia zilizopita? Hatujaachwa kwa kisio kuhusu umuhimu kama huo. Historia na unabii, vimeunganishwa kuwa pam-oja kwa kutoa mwanga wa ajabu na taratibu, katika matukio ya kutet-emesha dunia yalio karibu sana na ulimwengu mzima. ❑